

*Kupata Sauti ya Maelewana*



# MWONGOZO BAINIFU WA UKODISHAJI KATIKA VERMONT

IMETOLEWA KWA USHIRIKIANO NA



1-800-287-7971

1-802-864-0099

[www.cvoeo.org](http://www.cvoeo.org)



1-888-569-7368

1-802-985-2764

[www.vtlandlord.com](http://www.vtlandlord.com)

# UTANGULIZI

Ukodishaji unahusisha wahusika wawili. Njia bora zaidi kwa wamiliki na wapangaji kuwa na hali nzuri ya utumiaji ni kushirikiana. Ukodishaji pia ni uhusiano wa kisheria. Ukodishaji unafanikiwa zaidi ikiwa wahusika wote wawili watachukulia kama Uhusiano wa Biashara.

Mwongozo huu uliandikwa kwa pamoja mwaka wa 2015 na Pamela Favreau-Zugaro, Mkurugenzi wa zamani wa mpango wa Wapangaji wa CVOEO wa Vermont na Angela Zaikowski, Esq., Mkurugenzi wa Muungano wa Wapangishaji wa Vermont, na masasisho yalifanywa na CVOEO mnamo Agosti 2021 na Septemba 2023.

Kwa nini? Kwa sababu tunaamini kuwa uhusiano wa mmiliki/mpangaji si lazima uwe na ugomvi. Mawasiliano mazuri na kuheshimiana mara nyingi huepusha mfadhaiko kwa kila mhusika. Uzoefu umetuonyesha kuwa matatizo katika hali ya ukodishaji mara nyingi hutokana na wahusika wote wawili kutoelewa haki na wajibu wao wa kisheria. Mwongozo huu uliandikwa kwa ushirikiano na mashirika yetu kwa matumaini ya “kuleta haki na usawa kwa kila mhusika.” Tunaamini kwamba wahusika wote wawili wanapaswa kujua haki na wajibu wa kisheria wa mwingine pamoja na wao wenyewe.



## UJUMBE WETU KWA WAPANGAJI.

Lipa kodi yako ya nyumba kwa wakati na uwasiliane na mmiliki au msimamizi. Huwa tunasikia kutoka kwa wapangaji wengi wakifukuzwa kwa sababu hawakushughulikia mambo kwa wakati. Usiwe mmoja wao.

Masharti ya wamiliki wengi pia ni rahisi sana; wanatarajia ulipe kodi ya nyumba kwa wakati, utunze mali yao, na uwajulishe wakati ukarabati unapohitajika.

## UJUMBE WETU KWA WAMILIKI WA MALI

Nyumba ya ukodishaji ambayo haitunzwi na inayohitaji matengenezo na uboreshaji inaweza kuwa dhahirisho wazi kuwa haujali. Jiulize kwa nini wapangaji wako wanapaswa kuijali ikiwa haujali. Fahari ya Umiliki ni mbinu bora ya biashara.

Mahitaji mengi ya wapangaji pia ni rahisi; kufanyiwa matengenezo inapohitajika na kutosumbuliwa ili kufurahia nyumba yao.

# SHUKRANI

Toleo asili la Mwongozo huu liliwezekana kutokana na ruzuku kutoka kwa Shirika la Biashara na Maendeleo ya Jamii la Vermont (ACCD). Usaidizi wa kiufundi wa shirika unathaminiwa sana pia. Marekebisho na tafsiri ya mwaka wa 2023 ziliwezekana kutokana na ruzuku ya pili kutoka kwa ACCD pamoja na ufadhili wa ziada kutoka kwa Community Services Block Grant (CSBG) ya CVOEO na Ofisi ya Maendeleo ya Jamii na Uchumi ya Jiji la Burlington (CEDO).

# JEDWALI LA YALIYOMO

- 1 **SEHEMU YA 1. KABLA YA KUKODISHA**  
[Je, Sheria Zinatumiwa Kwangu?](#)
- 2 [Madokezo ya Wanaotafuta Nyumba](#)  
[Madokezo kwa Wamiliki](#)
- 3 [Kupitia Mambo Pamoja](#)
- 4 [Amana za Dhamana](#)
- 5 [Bima kwa Wahusika Wote Wawili](#)
  
- 6 **SEHEMU YA 2 – MAKUBALIANO YA UKODISHAJI**  
[Kutumia Mkataba Ulioandikwa kwa Ukodishaji](#)
- 7 [Ada za Kuchelewa na Ada za Faini](#)  
[Mikataba ya Ukodishaji Inayomfanya Mpangishaji](#)  
[Awajibikie Matengenezo](#)
- 8 [Mikataba ya Ukodishaji Inayozuia Wageni](#)  
[Vifungu vya Kusimamisha Mkataba wa Ukodishaji](#)
  
- 9 **SEHEMU YA 3 – ULINZI WA KISHERIA**
- 10 [Sheria ya Makazi ya Haki](#)
- 12 [Ubaguzi Kwa Msingi wa Hali ya Familia](#)
- 13 [Ubaguzi kwa Msingi wa Ulemavu](#)  
[Msaada kwa Watu Wanaoishi na Watu Walio na Ulemavu](#)
- 14 [Marekebisho Yanayofaa](#)
- 15 [Mabadiliko Yanayofaa](#)
- 16 [Utangazaji na Sheria ya Makazi ya Haki](#)
- 17 [Ulipizaji Kisasi Kinyume na Sheria](#)
- 18 [Haki za Faragha na Ufikiaji](#)
- 19 [Kuongezwa kwa Kodi ya Nyumba](#)
  
- 20 **SEHEMU YA 4 – KANUNI ZA MAKAZI**  
[Udhamini wa Uwezo wa Kukalika](#)
- 21 [Masharti ya Utiifu](#)
- 22 [Wadudu na Panya](#)
- 23 [Vipengele vya Kimuundo](#)
- 24 [Huduma za Nyumbani](#)  
[Usalama wa Moto](#)
- 25 [Rangi zenye Sumu ya Risasi](#)
- 27 [Kuweka Mali Katika Hali Nzuri](#)
- 28 [Kufanya Matengenezo na Kukata kwenye Kodi](#)  
[Kukataa Kulipa Kodi Hadi Matengenezo Yafanywe](#)
- 29 [Ikiwa Mmiliki Halipi Bili ya Huduma za Nyumbani](#)
  
- 30 **SEHEMU YA 5 – MATATIZO YA KAWAIDA**  
[Masuala kati ya Majirani](#)
- 31 [Utunzaji wa Nyasi na Uondoaji wa Theluji](#)  
[Maegesho](#)  
[Dishi za Setilaiti na Antena za Runinga](#)
- 32 [Kulipishwa Bili ya Huduma Zinzotumiwa](#)  
[Wengine Pia](#)
  
- 33 **SEHEMU YA 6 – KUHAMA**  
[Kuvunja Mkataba wa Ukodishaji](#)
- 34 [Masharti ya Notisi ya Wapangaji Wanaohama](#)  
[Matarajio ya Hali Wakati wa Kuhama](#)
- 35 [Marejesho ya Amana za Dhamana na Migogoro](#)  
[Vitu Vilivyoachwa Nyuma Baada ya Kuhama](#)
- 36 [Watu Wanaomfahamu Mhusika](#)
  
- 37 **SEHEMU YA 7 – USIMAMISHAJI WA UKODISHAJI UNAOFANYWA NA MMILIKI**  
[Usimamishaji wa Ukodishaji Kwa Kutolipa Kodi](#)
- 38 [Notisi ya Usimamishaji “Kwa Sababu Fulani”](#)
- 39 [Usimamishaji wa Ukodishaji “Bila Sababu”](#)  
[Notisi Wakati wa Kukodisha Ndani ya Makazi](#)  
[Binafsi ya Mmiliki](#)
- 40 [Notisi ya Mauzo ya Jengo](#)  
[Notisi ya Mmiliki Kushindwa Kulipa Rehani](#)  
[Kufukuza Wapangaji Ambao ni Wafanyakazi wa Shambani](#)
- 41 [Kipindi cha Mwisho wa Notisi](#)
  
- 42 **SEHEMU YA 8: MAHAKAMA UTARATIBU WA KUFUKUZWA**
- 43 [Istihali za Kufukuzwa](#)  
[Utaratibu wa Mahakama](#)
- 44 [Kesi ya Kulipa Kodi kwa Mahakama Badala ya Mpangishaji](#)
- 45 [“Malalamiko”](#)  
[“Jibu”](#)  
[Kesi ya Usikilizaji wa Mwisho](#)
- 46 [Amri ya Mahakama ya Kufukuzwa](#)  
[Vitu vya Mpangaji Baada ya Kufukuzwa](#)
  
- 47 **SEHEMU YA 9 – KUACHANISHA NYUMBA YA UKODISHAJI**  
[Mali Isiyodaiwa Baada ya Kuachanishwa kwa Nyumba](#)
  
- 48 **KIAMBATISHO CHA A:** [Zana](#)
- 72 **KIAMBATISHO CHA B:** [Nyenzo](#)

# SEHEMU YA 1: KABLA YA KUKODISHA

## JE, SHERIA HIZI ZINATUMIKA KWANGU?

“**Makubaliano ya ukodishaji**” inamaanisha makubaliano yote, yaliyoandikwa au ya mdomo, yanayo jumuishia sheria na masharti kuhusu matumizi na ukaaji kwenye nyumba na jengo.

“**Mpangishaji**” inaanisha mmiliki, mpangishaji, au inapotumika, mpangishaji mdogo wa nyumba ya makazi au jengo ambalo ni sehemu yake.

“**Mpangaji**” inaamisha mtu aliye na haki chini ya makubaliano ya ukodishaji ya kukaa kwenye nyumba ya makazi bila kujumuisha wengine.

Kwa ufupi, hii inamaanisha kwamba ikiwa utaruhusu mtu aishi katika jengo unalomiliki, iwe jumba la kifahari au chumba katika makazi yako mwenyewe, wewe ni **Mpangishaji**. Hii ni pamoja na mpangaji mkuu anayetoa mkataba mdogo kwa mwenzake wa chumba. Sio lazima uwe unamiliki chumba unachotoa mkataba mdogo ili kuchukua jukumu la mpangishaji.

Kwa sababu sheria ya Vermont haihitaji mkataba ulioandikwa wa upangishaji, unachukuliwa kuwa **Mpangaji** halali wa ukodishaji ukiwa na au bila mkataba wa upangishaji. Haki na wajibu wa wahusika wote wawili uliolezwa katika kitabu hiki unatumika.

[Sheria Zilizofafanuliwa za Vermont, Kichwa cha 9, Sura ya 137 § 4451. Ufafanuzi](#)

\* “V.S.A.” pia imetumiwa mara kwa mara katika kitabu hiki. Inamaanisha Sheria Zilizofafanuliwa za Vermont na inarejelea sheria za jimbo la Vermont. Inarejelewa na **KICHWA** (nambari fulani), **SURA** (mada ambayo inashughulikia), na **KIFUNGU** (maelezo mahususi ya sheria).

## HALI MAALUM

Maelezo yaliyo katika kitabu hiki hayatumiki kwa mojawapo ya yafuatayo:

- Ukaaji katika taasisi ya umma au ya binafsi inayoendeshwa kwa madhumuni ya kutoa huduma ya matibabu, matibabu ya wazee, elimu, ushauri, kidini au huduma kama hizo.
- Ukaaji chini ya mkataba wa uuzaji wa nyumba ya makazi au mali ambayo ni sehemu yake, ikiwa mkaaji ni mnunuzi au mtu anayeridhi maslahi ya mnunuzi.
- Ukaaji wa mshiriki wa shirika la kidugu, kijamii, au la kidini katika sehemu ya jengo linaloendeshwa kwa manufaa ya shirika.
- Ukaaji wa muda mfupi katika hoteli, moteli au nyumba za kupanga kwa muda wakati ukaaji huo unatozwa kodi ya vyumba na milo (siku 30).
- Ukaaji wa mmiliki kwenye kitengo cha miliki bia au mmiliki wa mkataba wa upangaji wa umiliki katika ushirika.
- Ukodishaji wa nyumba inayohamishika unaosimamiwa na [10 V.S.A. sura ya 153](#).
- Makazi ya muda mfupi katika uwanja wa kambi, ambayo kwa madhumuni ya kifungu hiki yanamaanisha mali yoyote inayotumika kwa ajili ya likizo ya msimu au ya muda mfupi au madhumuni ya burudani ambayo ndani yake kuna vijumba vya makuti, mahema, au maeneo ya kuegemea, au maeneo ya kambi yaliyoundwa kwa upigaji kambi wa muda au unaohamishika, burudani, au vitengo vya nyumba za usafiri, ikiwa ni pamoja na mahema, magari ya kambi, na magari ya burudani kama vile nyumba kwenye magari, trela za usafiri, lori za kambi na magari madogo ya kambi.


# MADOKEZO KWA WAPANGISHAJI NA WAMILIKI

## MADOKEZO KWA WANAOTAFUTA NYUMBA:

- Kuwa na uhakika unaweza kumudu kodi ya nyumba. Tumia [hati ya bajeti](#) katika sehemu ya “Zana” ya Mwongozo huu.
- Mmiliki au wakala wa ukodishaji hapaswi kutoza ada ya maombi.
- Uliza ikiwa kutakuwa na mkataba ulioandikwa wa ukodishaji. Uliza kuhusu urefu wa muda wa mkataba wa ukodishaji (muda wa mkataba wa ukodishaji).
- Uliza ni nani anayelipia huduma za nyumbani. Ikiwa utalipia gharama hizi, uliza kiasi chake. Pigia simu kampuni za huduma za nyumbani ili kuona ikiwa makadirio ambayo mmiliki alikupa ni sahihi.
- Ikiwa mmiliki analipa mfumo wa kupasha joto, uliza ni nani anayedhibiti halijoto ya nyumba.
  - Ikiwa ni mmiliki, uliza kuhusu kiwango cha halijoto kinachowekwa wakati wa msimu wa baridi. Nyumba za miliki bia zinahitaji halijoto isiyopungua 65°F.
- Usiogope kuwauliza watu wanaomfahamu mmiliki, waulize wakazi wa sasa kuhusu hali yao ya ukodishaji.
- Kagua mifumo yote muhimu:
  - Taa - Maji
  - Soketi - Jiko
  - Vigunduzi vilivyounganishwa vya moshi na kaboni monoksidi vinavyotumia umeme
- Watu wanaomfahamu mmiliki. Ikiwa unahisi hujaridhishwa na wanaomfahamu, [Vermont Tenants](#) inaweza kukusaidia. Wapigie simu.
- Baadhi ya wamiliki pia huangalia Ripoti ya Uwezo wa Kulipa Mkopo. Ikiwa huna uhakika kuhusu alama yako ya kuweza kulipa mkopo, au unahitaji usaidizi wa kujua au kuboresha alama hii ya kuweza kulipa mkopo, wasiliana na [Mpango wa Financial Futures](#) wa CVOEO ulioorodheshwa kwenye sehemu ya [Nyenzo](#) katika upande wa nyumba wa kitabu hiki.
- **Mkataba wa ukodishaji ni halali pindi tu unapotiwa saini, si baada ya kuhamia.**  
*Hakikisha unaclewa kile mkataba wa ukodishaji unasema kabla ya kuusaini!*  
*Wasiliana na [Vermont Tenants](#) ikiwa huna uhakika.*

## MADOKEZO KWA WAMILIKI:

- Wakati wa kutangaza nyumba, eleza kuhusu sifa za nyumba, wala sio sifa za wakaaji unaopendelea. Angalia pia kifungu kuhusiana na [Sheria ya Makazi ya Haki](#).
- Si halali kulipisha Ada za Maombi katika jimbo la Vermont.
- Unaweza kuomba kwamba mwombaji atoe nakala ya ripoti yake ya uwezo wa kulipa mkopo kama sehemu ya utaratibu wa kutuma ombi.
- Uliza watu wanaomfahamu! Maswali mazuri ya kuuliza ni pamoja na:
  - Kodi ya nyumba ilikuwa ikilipwa kwa wakati?
  - Je, mkodishaji alilipa malipo yote?
  - Je, ungemkodisha mtu huyu tena?
- Hakikisha kuwa matengenezo yoyote yanayohitajika yanafanywa kabla ya wapangaji wapya kuingia.
- Wakati wa kukataa ombi la mwombaji, unaweza kukataa waombaji kwa sababu zifuatazo:
  - Ombi ambalo halijakamilika
  - Maoni hasi kutoka kwa watu wanaomfahamu
  - Kukokuwa na historia ya kulipa kodi ya nyumba
  - Rekodi ya uhalifu
  - Alama isiyotosha ya kuweza kulipa mkopo - unaweza kuweka kiwango, lakini ukitumie kwa uthabiti
- Hakikisha unatumia sera zako zote za maombi kwa uthabiti.



# KUPITIA MAMBO PAMOJA

Wahusika wote wawili wanapaswa kupitia mambo pamoja kabla ya mpangaji kuanza kukaa. Kumbukumbu ya hali ya nyumba inapaswa kurekodiwa kwa maandishi. Kuna fomu zilizopo kwa kusudi hii [zinazopatikana kwenye sehemu ya “Zana” ya Mwongozo huu.](#)


## MADOKEZO KWA WAPANGAJI

Ikiwa mmiliki hatakagua mambo pamoja nawe au kuandika mambo:

- Piga picha kabla ya kuingia!
- Andika orodha ya vipengee vyote vilivyoharibika na vitu ambavyo vinapaswa kurekebishwa, unda nakala yake na uitume kwa mmiliki ukiomba vitu hivi vyote vitengenezwe.
- Hakikisha umeandika tarehe kwenye barua hiyo.
- Weka nakala yako mahali salama
- Kuwa mwangalifu unapoingiza samani. Ukikwaruza kuta au sakafu, mmiliki anaweza kukuwajibisha kwa uharibifu huo.

## MADOKEZO KWA WAMILIKI:

- Pitia mambo pamoja wakati wa kuingia ili kuwa na kumbukumbu ya hali ya nyumba.
- Mhitaji mpangaji asaini hati ya uthibitishaji wa kuhamia ili kuthibitisha hali ya nyumba.
- Piga picha au urekodi video ili kuwa na kumbukumbu ya hali hiyo wakati wa kuhamia.
- Iwapo wewe na mpangaji mnakubali kwamba matengenezo yanahitajika, fuatilia matengenezo haya (unaweza hata kumwomba mpangaji asaini hati akithibitisha kuwa matengenezo yamekamilika).



# AMANA ZA DHAMANA

Dhana ya kawaida kwamba mmiliki hawezi kuomba alipwe kodi ya mwezi wa kwanza, kodi ya mwezi wa mwisho na amana ya dhamana imekuwa ya kupotosha. Kwa kweli hii si sahihi. Burlington na Brattleboro ndizo pekee zimeweka amana ya dhamana isizidi kodi ya mwezi mmoja. Kwingineko katika jimbo, hakuna kikomo kwa kiasi cha amana.

- Sheria za Burlington na Brattleboro pia haziruhusu mmiliki akusanye zaidi ya nusu ya kodi ya mwezi mmoja kama amana ya mnyama kipenzi pamoja na amana ya dhamana.
- Sheria za Burlington pia zinahitaji mmiliki ahifadhi amana katika akaunti yenye riba. Riba hii hulipwa kwa mpangaji amana inaporejeshwa.
- Pesa zozote zinazolipwa mapema ili kupata upangaji zinaitwa “amana.” Hii ni pamoja na pesa za dhamana, uharibifu, usafishaji, amana za wanyama kipenzi, au kodi ya mwezi wa mwisho.
- Wamiliki hawaruhusiwi kutoza amana ya mnyama kipenzi kwa Mnyama wa Usaidizi anayehitajika kama Mabadiliko Yanayofaa kwa mpangaji aliye na ulemavu.
- Hakuna kitu kama amana “isiyoweza kurejeshwa”.
- Wapangaji hawapaswi kutumia amana kama kodi ya mwezi wa mwisho.
- Wamiliki wanaweza kukata pesa kutoka kwa amana kwa kodi ambayo haijalipwa, bili za huduma za nyumbani ambazo hazijalipwa, gharama ya kuondoa na kutupa vitu vya binafsi vya mpangaji, na uharibifu wa mali zaidi ya uchakavu wa kawaida.
- Amana haziwezi kuwekwa kama “faini” ya kuvunja mkataba wa ukodishaji.
- Amana zinaweza kushikiliwa chini ya mkataba wa ukodishaji ikiwa mpangaji ataondoka mapema na mmiliki hajaweza kukodisha tena nyumba hiyo.


## MADOKEZO KWA WAPANGAJI

Wakati wa ukaaji wako:

- Sheria ya Vermont – [9 V.S.A. sura ya 137 §4451\(5\)](#) inasema kwamba wapangaji wanaweza kuwajibishwa kwa "utelekezaji, upuuzaji, ajali au matumizi mabaya ya nyumba au vifaa au mali zisizohamishika yanayofanywa na mpangaji au wanafamilia wake au waalikwa au wageni wake.”
- Ripoti mahitaji ya matengenezo mara moja.
- Usifanye mabadiliko bila idhini iliyoandikwa ya mpangishaji.
- Tunza mali kwa heshima.
- Toa notisi inayofaa kabla ya kuhama. Kuna sampuli ya notisi kwenye sehemu ya [“Zana”](#) katika Mwongozo huu.
- Ukivunja mkataba wako wa ukodishaji kwa kuhama kabla ya muda wa mkataba wa ukodishaji kuisha, unaweza kuhitajika na mmiliki ulipe kodi isipokuwa na hadi mmiliki atakapoweza kukodisha tena nyumba hiyo.

## MADOKEZO KWA WAMILIKI:

- Hakikisha unakusanya amana na kodi zozote kabla ya wapangaji kuhamia kwenye nyumba.
- Ni rahisi zaidi kukata pesa za uharibifu wa nyumba wakati wapangaji wanaondoka ikiwa uliweka kumbukumbu ya hali hiyo wakati wa kuhamia ndani ya nyumba.



# BIMA KWA WAHUSIKA WOTE WAWILI

## UHARIBIFU KWA VITU VYA MPANGAJI

Uharibifu kwa vitu vya binafsi vya mpangaji kwa ujumla sio jukumu la mmiliki isipokuwa uharibifu ulisababishwa na utelekezaji wa mmiliki. Ikiwa nyumba yako itakosa uwezo wa kukalika kwa sababu ya moto, kupasuka kwa mabomba, nk, bima ya mpangaji italipia “gharama zako za ziada za maisha.” Kwa ujumla, hiyo inamaanisha bima itakulipia ili uishi mahali pengine, kama vile nyumba nyingine ambayo kodi yake inatoshana na ya nyumba yako ya asili.

Bima kawaida hulipia hasara kwa vitu vyako vya binafsi kutoka kwa aina 17 za hatari, ikiwa ni pamoja na: *moto au radi, dhoruba ya upepo au mvua ya mawe, mlipuko, ghasia au rabsha za umma, ndege, magari, moshi, uharabu au uharibifu wenye nia mbaya, wizi, uharibifu unaosababisha na kioo au nyenzo za ung'arishaji ambazo ni sehemu ya jengo, mlipuko wa volkano, vitu vinavyoanguka, uzito wa barafu, theluji au mvua ya theluji, uharibifu unaohusiana na maji kutoka kwa huduma za nyumbani na uharibifu wa kuongezeka kwa umeme.*


Huenda umegundua, hata hivyo, kwamba mafuriko na mitetemeko ya ardhi haziko kwenye orodha. Ikiwa unaishi katika eneo linalokabiliwa na hatari hizo, utahitaji kununua bima tofauti au bima ya nyongeza ya mpangaji. Katika baadhi ya maeneo ya pwani, ambapo vimbunga vinaweza kusababisha uharibifu mkubwa, unaweza pia kuhitaji kununua bima tofauti ya nyongeza kugharamia uharibifu wa dhoruba ya upepo.

## MADOKAZO KWA WAPANGAJI

- Inapendekezwa sana kwamba wapangaji wote wanunue bima ya mpangaji.
- Ikiwa mali ina tatizo ambalo halijashughulikiwa na linaweza kuhatarisha vitu vyako, tuma ombi la maandishi kwa mmiliki ukiomba tatizo hilo lishughulikiwe. Weka nakala ya ombi hilo.
- Matatizo ya kimsimu kama vile barafu inayoning'inia kwenye sehemu za maegesho kwa ujumla hazizingatiwi kama utelekezaji. Unafaa kuangalia kabla ya kuegesha. Kuwa na bima inayofaa ya gari.
- Ikiwa uharibifu wa vitu vyako unasababishwa na mpangaji mwingine, hilo sio jukumu la mmiliki.
- Angalia sehemu ya “Zana” kwa maelezo zaidi kuhusu [Bima ya Mpangaji](#).

## MADOKAZO KWA WAMILIKI:

- Mali yako inapaswa kuwa na bima ya kutosha ya nyumba na bima ya dhima.
- Shirikiana na wakala wako ili kuhakikisha kuwa una bima ya kutosha kulipia gharama ya jengo lingine.
- Kuwa na bima isiyotosha kunaweza kusababisha kampuni ya bima kutathmini faini ya kifedha wakati unapofanya dai.
- Ripoti mara moja madai ya mpangaji ya jeraha la binafsi au uharibifu wa mali kwa wakala wako. Kufanya hivyo kunaweza kukuepusha na kushtakiwa binafsi katika kesi.
- Angalia sehemu ya “Zana” kwa maelezo zaidi kuhusu [Bima ya Mali za Ukodishaji](#).






# SEHEMU YA 2: MAKUBALIANO YA UKODISHAJI

Ukodishaji ni uhusiano wa kisheria kati ya “Mpangishaji” (mmiliki) na “Mpangaji” (mkodishaji). Katika Vermont, haki na wajibu wa wahusika hawa wote wawili zinalindwa na sheria, hata kama hakuna mkataba ulioandikwa kwa ukodishaji.

Sheria ya Vermont hutumia maneno “Makubaliano ya Ukodishaji,” ambayo yanafafanuliwa kama “makubaliano yote, yaliyoandikwa au ya mdomo, yanayojumuisha sheria na masharti, kuhusu matumizi na ukaaji kwenye nyumba na jengo.” [9 V.S.A. §4451](#)

Aidha, sheria za VT zinaweka wazi kwamba hakuna makubaliano yaliyoandikwa ya ukodishaji (mkataba wa ukodishaji) yanayoweza kujumuisha lugha inayokiuka sheria hizi. Vifungu vyovyote kama hivyo vinachukuliwa kuwa visivyoweza kutekelezeka hata kama makubaliano yametiwa saini na wahusika wote wawili. Kifungu fulani kisichoweza kutekelezeka hakibatilishi mkataba wote wa ukodishaji. Vile vile, mhusika mmoja akivunja kifungu fulani katika mkataba wa ukodishaji haibatilishi mkataba wote wa ukodishaji. [9 V.S.A. §4454](#)



## KUTUMIA MKATABA ULIOANDIKWA KWA UKODISHAJI

Ni bora wakati wote makubaliano ya ukodishaji yawe katika maandishi. Inaepusha kutokuelewana baadaye. Wahusika wote wawili wanapaswa kuwa na ufahamu wazi kuhusu maana ya masharti haya ya mkataba wa ukodishaji.

## MATATIZO YANAPOTOKEA

Mkataba wa ukodishaji unaeleza matarajio ya wahusika wote wawili. *Kurasa zifuatazo zina madokezo kwa wahusika wote wawili wanaoingia katika makubaliano yaliyoandikwa ya ukodishaji.*

### MADOKOZO KWA WAPANGAJI

- Kamwe usitie saini mkataba wa ukodishaji hadi uwe umeusoma na umeuelewa kabisa.
- Unaweza kusaidiwa kukagua mkataba wa ukodishaji kwa kuwasiliana na [Vermont Tenants](#).
- Mkataba wa ukodishaji unakuwa halali unapoutia saini, SI tarehe ya kuhamia nyumba.
- Kuwa na uhakika kabla ya kusaini!
- Weka nakala yako mahali salama unapoweza kuufikia.
- Ikiwa mmiliki hatakupa nakala, iombe kwa maandishi na uhifadhi nakala ya barua hiyo ya ombi.

### MADOKOZO KWA WAMILIKI:

- Matumizi ya mkataba wa jumla wa ukodishaji kutoka kwenye intaneti au duka huenda usikufae kila wakati. Vifungu vya mkataba wa ukodishaji lazima viendane na sheria za jimbo ambapo ukodishaji wako uko.
- Unaweza kusaidiwa kukagua mkataba wa ukodishaji na [Muungano wa Wapangishaji wa Vermont \(Vermont Landlord Association\)](#).
- Mkataba wa ukodishaji unakuwa halali unapoutia saini, SI tarehe ya kuhamia nyumba.
- Mpe mpangaji wako nakala ya mkataba wa ukodishaji.
- Usiingie kwenye zaidi mkataba mmoja wa asili wa ukodishaji.

# ADA ZA KUCHELEWA NA ADA ZA FAINI

## MADOKEZO KWA WAPANGAJI

- Iwapo utatozwa ada ya kuchelewa unaweza kuomba hati kutoka kwa mmiliki inayotaja kwamba ada hiyo inahusiana na gharama anazotozwa kutokana na wewe kuchelewa kulipa kodi.
- Ikiwa mmiliki atashindwa kutoa hati hizi, huenda usihitajike kulipa ada hiyo.
- Kuna [barua kwa kusudi hili](#) katika sehemu ya “Zana” ya Mwongozo huu.

## MADOKEZO KWA WAMILIKI

- Unaweza kutoza ada ya kuchelewa ikiwa mpangaji halipi kodi kwa wakati ikiwa:
  - Ada ya kuchelewa inahusiana ipasavyo na gharama yako ya ukusanyaji. Hii inamaanisha kwamba ada hiyo inahitaji kuwa na uhusiano fulani na gharama ulizowekewa ikiwa mpangaji halipi kodi yake kwa wakati na/au inahusiana na muda unaotumia kumfuatilia mpangaji.
- Ada ya kuchelewa ambayo ni ada isiyobadilika kati ya \$20-\$25 kwa kawaida inakubalika.
- Ada ya kuchelewa inayohesabiwa kwa msingi wa idadi ya siku hairuhusiwi.
- Zingatia kutoa punguzo la malipo ya mapema badala ya ada ya kuchelewa. Punguzo la malipo ya mapema ni thawabu kwa mpangaji kwa kulipa kodi yake kabla ya muda wake wa kulipa (kinyume na faini ya kuchelewa kulipa).

# MIKATABA YA UKODISHAJI INAYOFANYA MPANGAJI AWAJIBIKIE MATENGENEZO

## MADOKEZO KWA WAPANGAJI

- Wapangaji hawapaswi kamwe kufanya matengenezo ambayo hayajaidhinishwa kwa maandishi na mmiliki.
- Wapangaji wala wamiliki hawapaswi kufanya matengenezo yanayohitaji fundi aliyeidhinishwa.
- Kifungu katika mkataba wa ukodishaji ambacho kinamfanya mpangaji kuwajibikia matengenezo hakiwezi kutekelezwa.

## MADOKEZO KWA WAMILIKI

- Wamiliki wanawajibikia kufanya matengenezo katika mali ya ukodishaji.
- Ikiwa kipengee kinachotengenezwa kiliharibiwa na mpangaji au wageni wake, unaweza kutafuta fidia kutoka kwa mpangaji.
- Wamiliki wanapaswa kudhibiti ni nani anayefanya matengenezo katika mali hiyo na jinsi matengenezo hayo yanafanywa.

# MIKATABA YA UKODISHAJI INAYOZUIA WAGENI

## MADOKEZO KWA WAPANGAJI

- Wamiliki hawapaswi kuingilia haki ya mpangaji ya kuwa na wageni anaopendelea.
- Wamiliki hapaswi kutoa notisi ya kuingia mali bila ruhusa kwa mgeni wa mpangaji.
- Ikiwa mtu anayekaa nawe ana makazi yake ya kudumu, yeye ni mgeni.
- Katika hali ambapo mgeni wako anatumia nyumba yako badala ya yake kama makazi ya msingi anaweza kuchukuliwa kuwa anaishi nawe.
- Ikiwa hana makazi yake ya kudumu, basi inachukuliwa kuwa anaishi nawe.
- Ukiruhusu mtu aishi nawe inaweza kuwa ngumu sana kumfanya aondoke. Huenda ukahitaji kufuata utaratibu wa kisheria wa kumfukuza.
- Unaweza pia kuhatarisha hali yako kama mpangaji. Kumruhusu mtu ambaye hajajumuishwa katika makubaliano ya ukodishaji na mmiliki aishi nawe ni msingi wa kusimamisha upangaji wako.

## MADOKEZO KWA WAMILIKI:

- Wamiliki hawawezi kudhibiti uwezo wa mpangaji kuwa na wageni; hata hivyo, wapangaji wanawajibika kwa tabia ya wageni wao.
- Inaweza kuwa vigumu kuunda sera ya wageni inayofaa na inayoweza kutekelezeka.
- Sera inayohitaji mpangaji kumjulisha mmiliki kuhusu wageni wote kwa kawaida huenda isiweze kutekelezeka.



# VIFUNGU VYA KUSIMAMISHA MKATABA WA UKODISHAJI

## MADOKEZO KWA WAPANGAJI

- Unawajibishwa kwa muda ulioelezwa kwenye mkataba wa maandishi wa ukodishaji.

Matokeo ya kuhama kabla ya mwisho wa mkataba wa ukodishaji:

- Mmiliki anaweza kukuwajibisha kifedha kwa kodi (na huduma za nyumbani, ikiwa ni jukumu la mpangaji) hadi mwisho wa mkataba wa ukodishaji au hadi mmiliki apate mpangaji mpya.
- Unaweza pia kuwajibika kwa gharama zinazohusiana na kukodisha tena nyumba.
- Kifungu cha mkataba wa ukodishaji kinachosema kuwa mmiliki anaweza kukuondoa bila utaratibu wa kisheria wa mahakama hakiwezi kutekelezeka.


## MADOKEZO KWA WAMILIKI:

- Ikiwa unataka mpangaji ahame, unahitaji kumtumia notisi ya kusimamisha mkataba - hata kama ni mwishoni mwa muda wa mkataba wa ukodishaji.
- Bila notisi halisi ya kusimamisha mkataba, huwezi kuanza hatua ya mahakama dhidi ya wakaaji - hata kama mkataba wako wa ukodishaji unasema wanapaswa kuhama mwishoni mwa muda wa mkataba huo wa ukodishaji.
- Ikiwa mpangaji wako ataondoka kabla ya mwisho wa muda wa mkataba wa ukodishaji, unaweza kumwajibisha kifedha alipe kodi ya nyumba, huduma za nyumbani (ikiwa mkataba unasema mpangaji ndiye atalipa) na gharama zinazofaa zinazohusiana na kukodisha tena nyumba hiyo.

## SEHEMU YA 3: ULINZI WA KISHERIA

Uhusiano wa ukodishaji unasimamiwa na sheria na zinatumiwa kwa kila mtu katika Vermont. Haki na wajibu mwingi, lakini sio wote, wa Mmiliki na Mpangaji huangaziwa katika [Kichwa cha 9 V.S.A. \(Sheria Zilizofafanuliwa za Vermont\) Sura ya 137.](#)

Hiyo haimaanishi kuwa suluhisho la kila hali linaweza kupatikana katika kifungu hicho cha sheria. Sheria ya Kawaida, Sheria za Kurejesha Umiliki, Sheria za Uhalifu, Sheria ya Makazi ya Haki na hata Sheria ya Maamuzi ya Mahakama hutumiwa wakati wa ukodishaji. Sio suluhu zote ziko wazi. Kuna sehemu nyingi tatanishi na hadithi nyingi za uwongo. Mbinu bora zaidi wakati wote ni kutafuta usaidizi wa kitaalamu.



# SHERIA YA MAKAZI YA HAKI

THE TIME IS ALWAYS RIGHT  
TO DO WHAT IS RIGHT  
MLK



## JE, MAKAZI YA HAKI NI NINI?

- Makazi ya Haki ni haki ya mtu kuchagua mahali anapoishi na haki ya kukodisha, kununua au kufadhili nyumba ya kuishi bila ubaguzi.
- Makazi ya Haki ni haki ya fursa sawa katika makazi.

## BAADHI YA MANENO YANAYOTUMIWA SANA:

- **“Aina Inayolindwa”** – aina za watu ambazo sheria ya Makazi ya Haki hutumika.
- **“Hali ya Familia”** – Uwepo wa watoto wadogo.
- **“Uelekezaji mbali”** – Kuelekeza mbali au kutoruhusu mshirika wa aina inayolindwa kufikia nyumba zote zinazopatikana za ukodishaji.  
Mfano - kupendekeza mtu anayetumia mikongojo/kiti cha magurudumu kwamba ghorofa ya kwanza inaweza kumfaa zaidi kuliko ghorofa ya pili aliyoomba kutazama.
- **“Ubaguzi Usiokusudiwa”** - Sheria isiyoegemea upande wowote ambayo ina athari kubwa kwa washiriki wa aina inayolindwa.

## MADOKAZO KWA WAMILIKI:

- Mmiliki ana haki ya kuanzisha na kutekeleza taratibu halali za biashara zinazohitajika ili kulinda na kudhibiti mali ya ukodishaji, kama vile kuhitaji watu wanaomfahamu mpangaji au kukataa kukodisha kwa watu ambao hawana mapato ya kutosha kulipa kodi ya nyumba. Hata hivyo, masharti haya lazima yatumike kwa uthabiti kwa watu wote.
- Wamiliki pia wanaweza kukataa kukodisha kwa watu walio na historia ya tabia isiyofaa katika ukodishaji wa awali, kama vile kusumbua wakazi wengine, kuharibu mali au kutolipa kodi.
- Wamiliki, hata hivyo, hawapaswi kutumia mbinu za biashara halali kama kisingizio cha ubaguzi.
- Ni kinyume na sheria kwa mmiliki kuuliza mkodishaji au mpangaji mtarajiwa ikiwa ana ulemavu. Hata hivyo, ikiwa mpangaji mwenye ulemavu anaomba mabadiliko yanayofaa, mmiliki ana haki ya kuomba uthibitisho wa ulemavu huo na hitaji la mabadiliko yaliyoombwa, isipokuwa kama ulemavu huo ni dhahiri. Mmiliki hapaswi kuuliza ulemavu ni mgani.

## AINA 13 ZINAZOLINDWA

### ULINZI WA SHIRIKISHO

Mbari	Hali ya Familia
Rangi	Ulemavu
Dini	Jinsia
Asili ya Taifa	

### ULINZI ZAIDI WA VERMONT

Umri (18+)
Hali ya Ndoa (waliofunga na wasiofunga ndoa)
Mwelekeo wa Jinsia
Utambulisho wa Jinsia
Upokeaji wa Msaada wa Serikali
Waadhiriwa wa dhuluma, unyanyasaji wa kingono au unyatiji



## UBAGUZI WA MAKAZI NI ZOZOTE KATI YA SHUGHULI ZIFUATAZO KWA MSINGI WA KUWA MSHIRIKA WA AINA INAYOLINDWA:

- Kukataa kukodisha, kuuza au kufadhili makazi.
- Kuweka sheria, masharti, au haki tofauti au kutoa huduma au vifaa tofauti vya makazi.
- Kuunda, kuchapisha nakala halisi, au kuchapisha notisi, taarifa, au tangazo lolote linaloonyesha upendeleo, kizuizi au ubaguzi wowote.
- Kutoa maelezo ya uwongo kuhusu upatikanaji wa mauzo, ukaguzi au ukodishaji.
- Kunyima mtu yeyote ufikiaji wa kituo au huduma inayohusiana na uuzaji au ukodishaji nyumba (MLS, shirika la mawakala wa mali isiyohamishika, n.k.).
- Kulazimisha, kutishia, au kuingilia mtu yeyote katika makazi au kwa sababu ya kufungua au kuunga mkono mashtaka ya ubaguzi.

[Sheria Zilizofafanuliwa za Vermont, Kichwa cha 9, Sura ya 139](#)

## JE, MALI INASHUGHULIKIWA NA SHERIA HII?

- Sheria ya haki ya makazi inatumika kwa makazi ya kuishi na si mali za biashara kama vile maduka ya rejareja na ofisi. Mali za kibiashara zinashughulikiwa chini ya sheria ya makazi ya umma.
- Mbari, rangi na asili ya taifa hushughulikiwa katika matukio yote, hata kama mali hiyo haishughulikiwi.
- Utangazaji na taarifa za umma pia wakati wote hushughulikiwa na sheria ya makazi ya haki.

Sheria ya Vermont hutoa **hali maalum chache sana** kwa sehemu nyingine za sheria ya makazi ya haki. *Hata kama mali hiyo haishughulikiwi na sheria, masharti ya utangazaji na ubaguzi kwa misingi ya mbari, rangi na asili ya taifa hushughulikiwa kila wakati.*

- Majengo yenye nyumba tatu au chini hayashughulikiwi, lakini tu ikiwa mmiliki au mwanafamilia wa karibu wa mmiliki anaishi katika moja ya nyumba. (Katika jiji la Burlington, hali maalum inatumika tu kwa majengo yenye nyumba mbili.)
- Kukataa kumkodisha mpangaji anayeweza kuwa chini ya umri wa miaka 18 inakubalika.
- Upendeleo wa kidini unaotolewa kwa wapangaji wa dini sawa na ule wa ushirika wa kidini ambao hutoa au kukodisha vyumba bila faida haukubaliki.
- Nyumba za kukodisha kwa wazee ambazo zinabagua familia zilizo na watoto zinakubalika ikiwa ni watu walio na umri wa zaidi ya miaka 62 pekee wanaokaa katika makazi hayo na, au ikiwa angalau mtu mmoja aliye na zaidi ya umri wa miaka 55 anaishi katika kila nyumba na jengo linatoa vifaa na huduma muhimu au fursa muhimu za makazi kwa wazee.
- Kukodisha nyumba ambazo zitakuwa ndogo sana kwa familia inayotaka kuishi huko, kulingana na viwango vinavyotumika vya upangaji, ni kinyume na sheria.

## UBAGUZI KWA MSINGI WA HALI YA FAMILIA

- Makazi hayawezi kunyimwa na sheria au masharti tofauti hayawezi kutumika kwa sababu ya uwepo wa watoto wadogo.
- Familia haziwezi kuelekezwa mbali na (au kuelekezwa kwa) na nyumba au mali fulani.
- Sheria zinapaswa kutumika kwa uthabiti kwa wapangaji wote na sio kwa familia zilizo na watoto pekee.
- Viwango vinavyofaa vya ukaaji vinaruhusiwa.

*Je, nini kinachukuliwa kuwa kiwango kinachofaa cha ukaaji?*

- Kama kanuni ya jumla, viwango vya ukaaji vinavyoweka kikomo cha watu wawili kwa kila chumba cha kulala au eneo la kulala lililoidhinishwa (vyumba vilivyo ndani ya nyumba vinavyotumika kulala lazima vizingatie masharti ya Usalama wa Moto), au kufuata Vikomo vya Ukaaji vya Manispaa au kibali cha mali kinachoweka kikomo cha idadi kwa ukaaji havikiuki sheria ya makazi ya haki.
- Sheria zinazoweka kikomo cha idadi ya watoto kwa kila nyumba badala ya idadi ya watu kwa kila nyumba ni za kibaguzi.
- Wakati wa kukagua kesi za ukaaji, [HUD](#) na [Tume ya Haki za Binadamu ya Vermont](#) huzingatia ukubwa na idadi ya vyumba vya kulala na hali zingine maalum.



## MADOKEZO KWA WAMILIKI

- Ni uamuzi wa wazazi ikiwa wanataka watoto (ikiwa ni pamoja na watoto wa jinsia tofauti) kulala chumba sawa.
- Sheria zinazohusiana na kelele lazima zizuie kila mtu kutoa sauti kubwa zisizo za lazima, sio watoto tu.
- Tunga sheria zinazotumika kwa kila mtu.
- Toa huduma au manufaa yanayotumika kwa kila mtu, ikiwa ni pamoja na watoto.
- Tangaza au ueleze nyumba jinsi ilivyo, badala ya nani atakuwa mwombaji unayependelea.
- Epuka maneno kama vile: “inafaa kwa watu wasiofunga ndoa” au “mahali pazuri kwa watu wawili” kwani haya yanaweza kufasiriwa kama kujaribu kuwatenga watoto.

# UBAGUZI KWA MSINGI WA ULEMAVU

## KUFAFANUA ULEMAVU

Mtu anachukuliwa kuwa na ulemavu ikiwa mojawapo ya vigezo vitatu vifuatavyo inatumika:

- Matatizo ya kimwili au kiakili ambayo yanazuia kwa kiasi kikubwa utendakazi mmoja au zaidi wa maisha.
- Mtu ambaye anachukuliwa na wengine kuwa na matatizo kama hayo.
- Kumbukumbu ya kuwa na ulemavu - K.m. risiti ya SSI, SSDI, nk.

“Ulemavu wa kimwili au kiakili” unarejelea *hali au ugonjwa unaoathiri akili au mwili.*

“Unaozuia kwa kiasi kikubwa” inarejelea *kwa kipindi kirefu cha muda au kwa kiasi kikubwa.*

“Utendakazi mmoja au zaidi wa maisha” unarejelea *kutembea, kuzungunza, kupumua, kuona, kusikia, kujitunza, kulipa bili, nk.*

[-V.S.A. Kichwa cha 9, Sura ya 139](#)

## MSAADA KWA WATU WANAOSHISHI NA WATU WALIO NA ULEMAVU

- Mtu mwenye ulemavu ana haki ya kuomba msaada wa mtu anayeishi na mtu mlemavu.
- Mapato na mali ya mtu anayeishi na mtu mlemavu haihesabiwi dhidi ya miongozo ya mapato ya msaada wa makazi ya umma.





# MAREKEBISHO YANAYOFAA KWA WAKAAJI WENYE ULEMAVU

## JE, MAREKEBISHO YANAYOFAA NI NINI?

- Mabadiliko halisi kwa jengo au nyumba ya kukodisha ambayo huruhusu wakaaji walemavu kupata matumizi na starehe sawa na mtu asiye na ulemavu.
- Marekebisho katika nyumba zenye ruzuku ya serikali kawaida hulipiwa na mmiliki.
- Marekebisho katika nyumba binafsi za ukodishaji kawaida hulipiwa na mkaaji.
- Mkaaji anaweza kuhitajika kurejesha nyumba katika hali yake ya asili wakati wa kuondoka ikiwa mmiliki ataomba.

## MIFANO YA MAREKEBISHO YANAYOFAA:


- Kupanua milango ili kufanya iwe rahisi zaidi kuingia kwenye vyumba.
- Kuweka fito za kushikia katika bafu.
- Kupunguza urefu wa makabati ya jikoni ili kufaa mtu anayetumia kiti cha magurudumu.
- Kuweka njia panda ya viti vya magurudumu kwenye sehemu ya nje ya jengo.
- Kigunduzi cha moshi na kaboni monoksidi ambacho kinamweka.

## KUOMBA MAREKEBISHO YANAYOFAA

Chini ya Sheria ya Makazi ya Haki, mmiliki hapaswi kumhitaji mpangaji atumie fomu mahususi au hata kuhitaji ombi hilo liwe kwa maandishi. Hata hivyo, Vermont Tenants inapendekeza sana kwamba maombi yote yafanywe kwa maandishi kwa madhumuni ya kumbukumbu. Wapangaji wanaweza kupata usaidizi kuhusu maombi kwa kuwasiliana na [Mradi wa Makazi ya Haki wa CVOEO](#) au huduma zingine zilizoordheshwa nyuma ya mwongozo huu. Pia kuna [sampuli za barua](#) katika sehemu ya “Zana” ya Mwongozo huu.

## MADOKAZO KWA WAMILIKI:

- Ombi la mabadiliko au marekebisho yanayofaa linaweza kufanywa kwa maneno au kwa maandishi na linaweza kutoka kwa mtu mwenye ulemavu au mtu anayetenda kwa niaba yake.
- Lazima utoe jibu la haraka kwa maombi yote ya mabadiliko au marekebisho yanayofaa.
- Unaweza kuomba mkaaji atoe maelezo yanayofaa ya marekebisho anayopendekeza.
- Unaweza kumwomba mkaaji kazi hiyo ifanywe na mtu mwenye mafunzo ya kikazi.
- Unaweza kuomba mkaaji apate vibali vyote husika kabla ya kuanza urekebishaji.
- Usimhitaji mkaaji alipe amana ya ziada.
- Mombi ya marekebisho na mabadiliko yanayofaa huwa na ukweli mahususi na yanaweza kuhitaji uchanganuzi kulingana na kila hali.
- Maombi ya marekebisho au mabadiliko yanayofaa yanapaswa kujadiliwa na wakili wako ikiwa huna uhakika kama unapaswa kuyakubali au la.



# MAREKEBISHO YANAYOFAA KWA WAKAAJI WALEMAMU

## JE, MABADILIKO YANAYOFAA NI NINI?

Mabadiliko kwa sheria, sera au mbinu ambayo huruhusu mkaaji mlemavu fursa sawa ya kutumia na kufurahia nyumba ya makazi.

## JE, “YANAYOFAA” INAMAANISHA NINI?

- “Yanayoonekana kufaa kwa uhalisia wake” au ikiwa ombi linaonekana kuwa linawezekana au kukubalika
- Ikiwa ombi litasababisha mabadiliko ya kimsingi katika biashara ya mmiliki au lina mzigo mkubwa wa kifedha kupita kiasi (Ugumu Usiofaa), huenda ombi hilo lisilazimike kukubaliwa.

## JE “UGUMU USIOFAA” UNAMAANISHA NINI?

- Ombi litasababisha ugumu au gharama kubwa kwa mmiliki.
- Ugumu usiofaa haurejelei tu ugumu wa kifedha, bali pia maombi ambayo yanahitaji mabadiliko ya kina, makubwa, au yanayovuruga, au yale ambayo kimsingi yatabadilisha asili au uendeshaji wa biashara.

## MIFANO YA MABADILIKO YANAYOFAA

- Mkaaji aliye na ulemavu wa kimwili au kiakili anaomba marekebisho ya sera ya “Hakuna Mnyama Kipenzi” ili apate nafasi ya kuwa na mnyama wa usaidizi anayemsaidia katika ulemavu wake (hakuna mafunzo maalum yanayohitajika).
- Mkaaji aliye na tatizo la kutembea anaomba atengewe au ahamishiwe maegesho kwenye nafasi iliyopo karibu na mlango wake wa kuingilia, hata kama mali hiyo haina nafasi za maegesho zilizotengwa.
- Mkaaji aliye na msaidizi anaomba nakala ya ziada ya funguo ili kuruhusu aingie nyumba yake kwa urahisi.
- Mkaaji mwenye uraibu na sasa anapona anaomba kuzingatiwa kwa mabadiliko kwenye miongozo ya maombi licha ya kuwa na rekodi ya uhalifu kutokana na uraibu wake.

## KUOMBA MABADILIKO YANAYOFAA

Chini ya Sheria ya Makazi ya Haki, mmiliki hapaswi kumhitaji mpangaji atumie fomu mahususi au hata kuhitaji ombi hilo liwe kwa maandishi. Hata hivyo, Vermont Tenants inapendekeza sana kwamba maombi yote yafanywe kwa maandishi kwa madhumuni ya kumbukumbu. Wapangaji wanaweza kupata usaidizi kuhusu maombi kwa kuwasiliana [na Mradi wa Makazi ya Haki wa CVOEO au huduma zingine zilizoorodheshwa nyuma ya mwongozo huu. Pia kuna sampuli za barua katika sehemu ya “Zana” ya Mwongozo huu.](#)

## MADOKEZO KWA WAMILIKI:

- Jibu maombi yote kwa wakati ufaao.
- Maswali ambayo **hupaswi** kuuliza:
  - Je, mkaaji ana ulemavu wa aina gani.
  - Maswali ambayo yatahitaji kufichuliwa kwa historia ya matibabu.
  - Ikiwa mtu huyo anaweza kuishi kwa kujitegemea.
- Maswali unayoweza kuuliza:
  - Uthibitishaji kwamba mkaaji ana ulemavu, lakini tu ikiwa ulemavu hauonekani wazi.
  - Marekebisho au mabadiliko ambayo mkaaji anaomba.
  - Kuna uhusiano gani kati ya ulemavu na marekebisho au mabadiliko hayo mahususi.
- Unaweza kuunda fomu na utaratibu wa kushughulikia maombi ya marekebisho/mabadiliko yanayofaa, lakini haupaswi kumhitaji mkaaji atumie fomu hiyo kutuma ombi.

## MADOKEZO KWA WAPANGAJI

- Pata taarifa kutoka kwa daktari wako au mtaalamu aliyeidhinishwa inayothibitisha kwamba wewe ni ulemavu na kwamba unahitaji mabadiliko au marekebisho kwa sababu ya ulemavu huo.
- Tumia maneno kama vile “Marekebisho Yanayofaa” au “Mabadiliko Yanayofaa” kwenye ombi lako.
- Ikiwa mmiliki atakataa kutii ombi lako, unaweza kuwasiliana na [Mradi wa Makazi ya Haki](#) au [huduma zingine zilizoorodheshwa upande wa nyuma wa Mwongozo huu](#) kwa usaidizi.

# UTANGAZAJI NA SHERIA YA MAKAZI YA HAKI

## SHERIA YA VERMONT INASEMA NINI:

*“Itakuwa ni kinyume na sheria kwa mtu yeyote ... kuunda, kuchapisha nakala halisi, au kuchapisha mtandaoni, au kusababisha kuundwa, kuchapishwa kwa nakala halisi, au kuchapishwa mtandaoni notisi, taarifa, au tangazo lolote, kuhusiana na uuzaji au ukodishaji wa nyumba au mali nyingine linaloonyesha upendeleo, kizuizi, au ubaguzi wowote kwa misingi ya mbari, jinsia, mwelekeo wa kijinsia, utambulisho wa kijinsia, umri, hali ya ndoa, imani ya kidini, rangi, asili ya taifa, au ulemavu wa mtu, au kwa sababu mtu ana nia ya kukaa pamoja na mtoto mmoja au zaidi, au kwa sababu mtu ni mpokeaji wa msaada wa serikali, au kwa sababu mtu ni mwathirika wa dhuluma, unyanyasaji wa kingono au unyatiaji.”*

[9 V.S.A. Sura ya 139 §4503](#)

- Wakati wa kutoa matangazo au kumnyima mwombaji, mpangishaji hapaswi kutumia maneno au kauli za kibaguzi.
- Mifano ya Maneno ya Kibaguzi:
  - Makazi ya kikiristo
  - Watu waliokomaa
  - Haiwezi kufikiwa na walemavu
  - Inafaa kwa watu wasiofunga ndoa
  - Hakuna wanyama kipenzi, hakuna hali za kipekee
  - Sehemu ya 8 hairuhusiwi

## VIGEZO VINAVYORUHUSIWA VYA UCHUNGUZI WA MPANGAJI:

- Ameonyesha uwezo wa kulipa kodi kwa wakati.
- Watu wanaomfahamu kwa mpangishaji na/au binafsi.
- Ukaguzi wa uwezo wa kulipa mkopo, ikijumuisha masharti ya alama ya chini zaidi ya uwezo wa kulipa mkopo.
- Historia ya uhalifu.
- Mwombaji anaweza kuomba fursa ya kueleza hali yoyote mbaya.
- Ombi la marekebisho yanayofaa na mwombaji haliwezi kuwa msingi wa kukataa kumkodishia.

## MADOKEZO KWA WAMILIKI

- Eleza jinsi nyumba inavyokaa, si aina ya mkaaji unayetafuta.
- Kumbuka kwamba huwezi kumnyima mtu fulani nyumba katika aina inayolindwa isipokuwa kuna sababu nyingine halali kama vile historia duni ya kulipa mikopo au ikiwa nyumba hiyo tayari imekodishwa.
- Kagua utangazaji wote ambao wengine wanatangaza kwa niaba yako - ikiwa mkaaji wa sasa anatangaza ili kupata mkodishaji mdogo au mpangishaji mwenza, mmiliki anaweza kuwajibishwa kwa kauli za kibaguzi zinazotumiwa.

## MADOKEZO KWA WAPANGAJI WANAOFIKIRI WANABAGULIWA

- Tofauti kati ya **Ubaguzi** na **Ubaguzi ulio Kinyume na Sheria**
  - Kukataa kukukodisha kwa sababu una chale au vipuli au historia ya uhalifu kunaweza kuwa ubaguzi, lakini si Ubaguzi Kinyume na Sheria kwa sababu hakuna hata moja kati ya hizi inayochukuliwa kuwa “aina inayolindwa.”
  - Kukataa kukukodisha kwa sababu una alama mbaya ya kulipa mikopo au marejeleo yasiyofaa, hata kama wewe ni mlemavu, hakuchukuliwi kuwa Ubaguzi Kinyume na Sheria.
  - Kuweka sheria au sera tofauti kwa sababu ya tabia yako hakuchukuliwi kuwa ubaguzi mradi tu tabia hiyo haitokani na ulemavu wako au haihusiani na kuwa mshiriki wa aina inayolindwa.

# ULIPIZAJI KISASI KINYUME NA SHERIA

## SHERIA YA VERMONT INASEMA NINI:

Ni kinyume na sheria kwa mmiliki kulipiza kisasi dhidi ya mpangaji ambaye ameomba mabadiliko au marekebisho yanayofaa au analalamika kuhusu ukiukwaji wa haki zake chini ya sheria ya Makazi ya Haki.

Aidha, mmiliki wa nyumba ya makazi hapaswi kulipiza kisasi kwa kuanzisha au kubadilisha masharti ya makubaliano ya ukodishaji, kuongeza kodi ya nyumba au kwa kuchukua au kutishia kuchukua hatua dhidi ya mpangaji ambaye:

- Amelalamika kwa shirika la serikali lililo na jukumu la kutekeleza sheria ya jengo, makazi, au afya kwa ukiukaji husika kwenye jengo unaoathiri sana afya na usalama;
- Amelalamika kwa mpangishaji kwa ukiukaji wa Sheria za Makubaliano ya Makazi ya Kukodisha au Sheria ya Makazi ya Haki ya Vermont; au
- Amepanga au amekuwa mwanachama wa muungano wa wapangaji au shirika kama hilo.

Ikiwa mpangishaji atachukua hatua kinyume na kifungu hiki, mpangaji ana haki ya kutafuta fidia ya uharibifu na ada zinazofaa za wakili na ana utetezi dhidi ya hatua yoyote ya kulipiza kisasi kwa ukaaji.

Ikiwa mpangishaji atatoa notisi ya kusimamisha ukodishaji kwa misingi yoyote isipokuwa kwa kutolipa kodi ndani ya siku 90 baada ya notisi ya huluki yoyote ya manispaa au ya serikali ya Jimbo kwamba jengo halizingatii kanuni husika za afya au usalama, kuna dhana inayoweza kupingwa kwamba usimamishaji wowote wa ukodishaji na mpangishaji ni ulipizaji kisasi kwa mpangaji kwa kuripoti ukiukaji wa sheria. (Mahakama itachukulia kuwa hatua ya kufukuzwa ni ulipizaji kisasi lakini mmiliki anaweza kujaribu kuthibitisha kuwa ni kwa sababu nyingine halali.)

[9 V.S.A. Sura ya 137 §4465](#)

## MADOKEZO KWA WAMILIKI:

- Ikiwa mpangaji atawasilisha malalamiko juu ya hali ya nyumba ya kukodisha, kagua nyumba hiyo na ufanye matengenezo yoyote yanayofaa. Usipuuze malalamiko ya mkaaji wa nyumba yako.
- Usimpe mpangaji wako notisi ya kusimamisha upangaji mara tu mpangaji atakapokulalamikia. Ikiwa mpangaji anakataa kulipa kodi kihalali, tafuta ushauri wa kisheria.

## MADOKEZO KWA WAPANGAJI

- Sio aina zote za kulipiza kisasi zinachukuliwa kuwa kinyume na sheria.
- Chini ya sheria ya Vermont, wamiliki hawatakiwi kuweka kodi sawa kwa nyumba sawa (isipokuwa katika Maeneo ya Nyumba Zinazoweza Kuhamishika).
- “Upangishaji” sio taaluma inayodhibitiwa; hawashurutishwi na sheria za usiri au maadili.
- Ikiwa una wasiwasi kuwa unalipizwa kisasi kinyume na sheria, wasiliana [Vermont Tenants](#) kwa ufafanuzi na usaidizi wa hali hiyo.

# HAKI ZA FARAGHA NA UFIKIAJI

## HIVI NDIVYO MMILIKI ANAVYOWEZA KUPATA UFIKIAJI WA NYUMBA YA MPANGAJI HUKU AKIHESHIMU HAKI YAKE YA FARAGHA :

### VIPI

- Kwa idhini ya mpangaji, ambayo haitazuiliwa bila sababu.
- Baada ya kumpa mpangaji noti ya angalau saa 48 kwa kuingia kati ya saa 9 a.m. na 9 p.m.
- Katika hali za dharura

### KWA NINI

- Ili kukagua jengo.
- Ili kufanya mabadiliko au matengenezo.
- Ili kutoa huduma zilizokubaliwa.
- Ili kuwaonyesha nyumba wapangaji au wanunuzi watarajiwa
- Ili kuepuka uharibifu wowote katika haki ya dharura.

## MADOKEZO KWA WAMILIKI:

- Kuingia katika nyumba ya mpangaji bila kufuata sheria ni “Uingiaji Bila Ruhusa Kinyume na Sheria,” kosa la uhalifu.
- Noti kwa mpangaji kwa uingiaji sio lazima iandikwe (inapendekezwa, lakini haihitajiki). Simu, ujumbe wa SMS, au barua inayoachwa kwenye mlango zinatoshwa.
- Ikiwa umetoa noti inayofaa, unaweza kuingia kwenye nyumba hata kama mpangaji hayuko nyumbani.

## MADOKEZO KWA WAPANGAJI

- Wapangaji hawapaswi kukataa “bila sababu” kutoa ruhusa ya kuingia.
- Ikiwa mmiliki ataingia kwenye nyumba yako bila noti anza kwa kumweleza sheria inavyosema. Kuna [barua kwa kusudi hili](#) katika sehemu ya “Zana” ya Mwongozo huu.
- Ikiwa mmiliki anaendelea kuingia, unaweza kupiga simu polisi.
- Katika hali mbaya zaidi, unaweza kutoa Noti ya Kuingia Bila Ruhusa dhidi ya mmiliki. Pigia [Vermont Tenants](#) kwa usaidizi kabla ya kufanya hivi



# KUONGEZWA KWA KODI YA NYUMBA

Ongezeko la kodi litaanza kutumika siku ya kwanza ya kipindi cha kukodisha kufuatia notisi iliyoandikwa kwa si chini ya siku 60 kwa mpangaji.

Mfano:

- Mpangaji analipa kodi yake siku ya kwanza ya kila mwezi. Tarehe ya kwanza ya mwezi hadi tarehe ya kwanza ya mwezi unaofuata ndicho Kipindi cha Ukodishaji.
- Mmiliki anampa mpangaji notisi iliyoandikwa ya ongezeko la kodi mnamo Juni 10. Si chini ya “Vipindi viwili Kamili vya Ukodishaji” inamaanisha ongezeko hilo litaanza kutumika tarehe 1 Septemba.
- Notisi haipaswi kuwa chini ya siku 60 ikiwa mpangaji hulipa kila wiki au mara mbili kwa mwezi.
- Sheria za jiji la Burlington zinahitaji muda wa notisi wa siku 90.
- Hakuna kikomo cha juu zaidi cha kiasi kinachoweza kuongezwa almradi kikomo hicho kimewekwa katika mkataba wa ukodishaji.

## MADOKEZO KWA WAMILIKI

- Kuongezwa kwa kodi kwa kawaida hakuwezi kufanywa wakati wa kipindi cha mkataba wa ukodishaji, kwa hivyo unaweza kuhitaji kupanga mapema.
- Mpangaji si lazima akubali ongezeko la kodi. Alimradi umetoa notisi inayofaa, iliyoandikwa ya ongezeko hilo, itaanza kutumika.
- Sehemu ya nyongeza ya mkataba wa ukodishaji, ambapo wapangaji hutia saini, panapendekezwa kwa nyongeza za muda wa ukodishaji na ongezeko la kodi ili kila mtu awe wazi kuhusu masharti haya.

## MADOKEZO KWA WAPANGAJI

- Ikiwa mmiliki hatakupa notisi iliyoandikwa au muda wa kutosha wa notisi, jibu kwa kumwandikia. Kuna [barua kwa kusudi hili](#) katika sehemu ya “Zana” ya Mwongozo huu.
- Urefu wa muda wa notisi umeundwa kwa ajili ya mpangaji kutoa notisi ya kutosha kwamba anakusudia kuhama badala ya kulipa nyongeza ya kodi.

# SEHEMU YA 4: KANUNI ZA MAKAZI

## UDHAMINI WA UWEZO WA KUKALIKA

Haki ya makazi salama imejikita katika sehemu ya sheria ya Vermont inayoitwa [Udhamini wa Uwezo wa Kukalika](#). Udhamini huu unamhitaji mmiliki kutoa na kudumisha jengo ambalo ni salama, safi na linalofaa kwa makao ya binadamu na kwa kufuata kanuni husika za makazi. Matatizo yoyote yanayoathiri afya au usalama katika nyumba ya kukodisha kwa ujumla ni ukiukaji wa udhamini huu.

Udhamini wa uwezo wa kukalika unadokezwa katika makubaliano ya ukodishaji kati ya mmiliki na mpangaji, iwe kwa mdomo au maandishi, na ulinzi chini ya udhamini huu hauwezi kunyimwa mpangaji kwa makubaliano yoyote ya maandishi au ya mdomo. Ikiwa mpangaji alifahamu au la kuhusu tatizo lililopo wakati wa kuhamia kwenye nyumba, ni wajibu wa mmiliki kurekebisha tatizo hilo.

Kwa ufupi, hii inamaanisha kuwa mkataba wa ukodishaji ulioandikwa hauwezi kutumika kumwajibisha mpangaji kwa matengenezo na nyumba zote za ukodishaji lazima zitii Kanuni za Afya na Usalama.

### KANUNI ZINAZOTUMIKA:

- Kanuni ya Afya ya Makazi ya Ukodishaji
- Kanuni ya Usalama wa Moto ya Vermont
- Kanuni za Maji taka/Ugavi wa Maji
- Sheria za Eneo

## WAJIBU WA JUMLA


### WAMILIKI

Hakuna mmiliki atakayekodisha kwa mwingine kwa ukaaji katika makao, nyumba ya makao, nyumba yenye wapangaji wengi, kitengo chenye wapangaji wengi, au nyumba inayohamishika ambayo haizingatii masharti ya kanuni hii. Ni wajibu wa mmiliki kudumisha majengo yote kwa kutii kanuni hii.

Mahakama Kuu ya Vermont imegundua kuwa Wapangishaji watakuwa wanakiuka sheria ya Ulinzi wa Mtumiaji ([9 V.S.A., Sura ya 63](#)) ikiwa watakodisha mali inayokiuka kanuni.

### WAPANGAJI

Mpangaji hatasababisha au kuchangia katika kutotii kanuni za nyumba ya makazi kwa vifungu husika vya kanuni za ujenzi, makazi na afya. [V.S.A. 9, 4456\(a\)](#)



# MASHARTI YA UTIIFU

## VIFAA VYA JIKONI:

- Nafasi ya kuhifadhi, kuandaa na kupakua chakula.
- Sinki ya jikoni.
- Sakafu na kaunta zisizofyonza viowevu.

## VIFAA VYA BAFU:

- Msala.
- Sinki.
- Hodhi au bafu la manyunyu.
- Sakafu isiyofyonza kiowevu
- Feni ya uingizaji hewa au dirisha.

## UGAVI WA MAJI/UTUPAJI WA MAJI TAKA:

- Ugavi wa kutosha wa maji moto na baridi.
- Halijoto ya maji moto kati ya 100°F na 120°F.
- Maji safi na salama ya kunywa.
- Mfumo unaofanya kazi vizuri wa tangi la maji machafu au maji taka.
- Mabomba katika hali nzuri ya kufanya kazi.

## HALI ZA TAKATAKA, TAKA NA USAFI:

- Vyombo vinavyodumu na safi vya kuweka taka, bidhaa zinazorejelezwa na mabaki ya vyakula vinavyotolewa na mpangishaji. Vyombo vya kuweka taka na mabaki ya vyakula lazima pia visipitishwe maji na viwe na vifuniko vinavyotoshea vizuri.
- Maeneo ya jumla ya usafishaji yanayotolewa na mpangishaji.
- Ikiwa mpangaji analipia kuondolewa kwa taka, mpangishaji lazima ahakikishe kuwa taka zinaondolewa kila wiki.
- Ikiwa jengo liko Burlington na kuna zaidi ya nyumba moja, mpangishaji lazima alipie kuondolewa kwa taka.

## MFUMO WA KUONGEZA JOTO:

- Vifaa vya mfumo wa kuongeza joto katika hali nzuri ya kufanya kazi na viwe vimekaguliwa ndani ya miaka 2 iliyopita (kitengo lazima kiwe na lebo ya sasa).
- Vifaa vya mfumo wa kuongeza joto vinapitisha hewa vizuri kwenda nje.
- Vifaa vya mfumo wa kuongeza joto vinavyoweza kuweka vyumba vyote vikiwa na halijoto ya zaidi ya 65°F bila kupasha joto kupita kiasi kwenye chumba ambacho kitengo cha mfumo wa kuongeza joto kimo.
- Ikiwa mpangishaji analipia gharama ya mfumo wa kuongeza joto, lazima upatikane wakati wowote wa mwaka halijoto ya nje ikiwa chini ya 55°F.

## UINGIZAJI HEWA WA ASILI NA WA KIMTAMBO:

- Kila chumba kinachoweza kukalika kina angalau dirisha au mlango mmoja, katika hali nzuri ya kufanya kazi ambao unaweza kufunguliwa kwa hewa safi.
- Skrini za dirisha zipo na zimefanyiwa matengenezo yanayofaa.
- Njia zote za ukumbi na ngazi katika maeneo ya jumla zina uingizaji hewa wa kutosha.
- Feni ya bafu, tundu la kutokea hewa, au dirisha linalotoa hewa moja kwa moja hadi nje.
- Kikaushio cha nguo kinachotoa hewa nje.

## TAA NA UMEME:

- Kila chumba kinachoweza kukalika, isipokuwa jikoni, kina angalau soketi mbili au soketi moja na mfumo mmoja wa taa unaofanya kazi.
- Jikoni ina angalau soketi mbili na mfumo mmoja wa taa unaofanya kazi.
- Soketi zilizo karibu na vyanzo vya maji ni vya aina ya GFCI.
- Viingilio vya jengo na maeneo ya jumla yana mwanga wa kutosha.
- Mifumo yote ya umeme imefanyiwa matengenezo inayofaa.
- Kazi ya umeme inafanywa na fundi umeme aliyeidhinishwa.



# WADUDU NA PANYA: JE, NANI ANAYEWAJIBIKIA UANGAMIZAJI HUU?

## MMILIKI ANAWAJIBIKA

- Maeneo ya jumla yasiyo na uvamizi wa wanyama (ikiwa ni pamoja na wadudu).
- Jengo lina muundo bora ili kuzuia wanyama wasiingie.
- Uvamizi katika zaidi ya nyumba moja.

## MPANGAJI ANAWAJIBIKA


- Uvamizi uko katika nyumba yao pekee.
- Uvamizi katika nyumba moja ya familia (isipokuwa wanyama walikuwepo wakati wa kuhamia).

*Ikiwa mwangamizaji anaweza kubaini asili ya wadudu/panya, mpangaji anaweza kuwajibika kifedha.*

## MAELEZO KUHUSU KUNGUNI

Kunguni ni wadudu wadogo ambao hunyonya damu ya binadamu. Kawaida hujitokeza usiku wakati watu wamelala. Kunguni huuma - lakini hawasambazi magonjwa. Kunguni hukunyonya damu bila maumivu, huku wakidunga kiasi kidogo cha mate katika utaratibu huo, ambayo inaweza kusababisha athari ya mzio mwepesi au mkali. **Kwa sababu hawabebi au kusambaza magonjwa, hawazingatiwi chini ya sheria ya Vermont kama sababu ya kukataa kulipa kodi.**

Kunguni wameongezeka sana tangu kupigwa marufuku kwa viuawadudu hatari kama vile DDT. Hawasababishwi na usafi mbaya au utunzaji mbaya wa nyumba. Wanaweza kutokea kwa mtu yeyote, popote. Hata hivyo, uwepo wao ni ukiukaji wa Kanuni ya Afya ya Makazi ya Kukodisha kama wadudu wengine wowote. Wapangaji wana jukumu la kisheria la kutowaleta katika nyumba ya ukodishaji na pia jukumu la kushiriki katika utaratibu wa kuwaangamiza. Kwa sababu hatua ya kuwaangamiza haitawamaliza kabisa, kuna hatua nyingi zinazohitajika ili kuondoa kunguni kwenye makao ambazo zinahitaji ushirikiano kutoka kwa mpangaji.



## WAJIBU WA MPANGAJI WAKATI WA KUANGAMIZA KUNGUNI

Fuata maagizo yote yanayotolewa na Kampuni ya Uangamizaji iliyopewa kazi hiyo na mpangishaji. Hii itajumuisha shughuli kama vile:

- Kusafisha na kupanga sebule.
- Kupunguza vitu vilivyotapakaa.
- Kuweka kwenye mifuko na kuondoa matandiko na mavazi.
- Kutumia kikaushio cha JOTO kwa dakika 30 kwa vifaa vya kuchezea vya nguo, viatu, makoti, mapazia, mikoba, nk.
- Kutenga mbali vitu safi hadi kunguni waishe.
- Kuzingatia kupata foronya za mito na shuka za kufunika godoro.
- Kusugua mikunjo ya godoro kwa brashi ngumu.
- Kutumia kivuta vumbi kwenye magodoro, fremu za kitanda, samani, sakafu na mazulia - hasa karibu na kitanda na nguzo za samani.
- Kuweka mfuko wa kivuta vumbi kwenye mfuko wa plastiki uliofungwa mara baada ya kuvuta vumbi.
- Kutupa mfuko uliofungwa kwenye chombo cha nje.
- Kusafisha vitani, mapazia, zulia, mazulia na nguo.
- Kuosha na kukausha matandiko na nguo kwenye mazingira yenye joto zaidi.

**Sio lazima utupe samani na magodoro. Zinapaswa kuwekwa dawa kama sehemu ya kazi ya kuangamiza wadudu.**

# KUEPUKA KUPATA NA KUENEZA KUNGUNI

- Kagua mizigo baada ya kwenda safari.
- Osha nguo za mchango kwenye mazingira ya joto zaidi kabla ya kuzivaa.
- Usichukue vitu vilivyotupwa mitaani.
- Kagua samani yoyote iliyotumika au kitu kingine cha ununuzi.
- Funga vitu vilivyoathiriwa kwenye mifuko ya plastiki kabla ya kuvitupa.
- Haribu kabisa vitu vilivyovamiwa ili kuzuia kutumiwa tena.
- Weka lebo kwenye vitu vilivyotupwa inayosema “imevamiwa na kunguni” ili kuzuia kutumiwa tena.

## MBINU BORA KWA WAPANGAJI

- Unaweza kuwajibika kifedha kwa kusababisha shambulio.
- Usichukue samani au nguo za bure zilizoachwa kando ya barabara.
- Ukisafiri, angalia malazi yako unapowasili na uangalie masanduku yako kwa uangalifu kabla ya kurudi.
- Nunua tu vitu vilivyotumika kutoka kwa wafanyabiashara ambao “huzisafisha kwa dawa” kabla ya kuuza.
- Ripoti kunguni wowote au wadudu wengine na panya kwa mmiliki mara moja.
- Ikiwa mmiliki hatashughulikia tatizo hilo, wasiliana na Afisa wa Afya wa Mji wako au Ofisi za Utekelezaji wa Kanuni za Jiji mara moja.

## MBINU BORA KWA WAMILIKI

Wamiliki wana wajibu wa kushughulikia mara moja wanapoarifiwa kuhusu uvamizi wowote, ikiwa ni pamoja na kunguni, na kuhakikisha kwamba taratibu sahihi za kuwaangamiza zinachukuliwa.

- Tumia mbinu jumuishi ya kushughulikia masuala ya wadudu, ikiwa ni pamoja na mbinu za kemikali na zisizo za kemikali kama vile kutumia joto na uondoaji wa vyanzo vya chakula.
- Tumia mtaalamu aliyeidhinishwa wa viuawadudu wa kibiashara. Kunyunyizia peke yako husambaza tu tatizo kwa nyumba zingine.

# VIPENGELE VYA KIMUUNDO

Vipengele vya kimuundo lazima vidumishwe katika hali na nzuri ya kufanya kazi. Vinapaswa kuwa na uwezo wa kuzuia upepo na mvua, kuzuia maji na kuzuia panya.

Mali lazima pia itunzwe ili isiwe na unyevu kupita kiasi au maji yasiyosonga mara kwa mara au kila baada ya muda ambayo yanaweza kusababisha ukuaji unaoonekana wa kuvu.

Ikiwa kuna kuvu, unyevu unaosababisha kuvu hiyo lazima uondolewe na kuvu isafishwe, au vifaa vya ujenzi vyenye unyevu viondolewe.

Sio lazima wala haipendekezwi ufanye upimaji wa kuvu. Hakuna viwango vya jimbo au shirikisho ambavyo vinaweza kutumika kulinganisha matokeo ya kipimo cha kuvu, na kwa hivyo matokeo ya kipimo kama hicho hayawezi kutumika kubainisha kama jengo ni “salama” au “si salama.” Kwa kawaida, kipimo kama hicho hakitoi taarifa yoyote ambayo inaweza kubadilisha hatua za kurekebisha tatizo.

- Msingi
- Ngazi
- Sakafu
- Kuta
- Dari
- Dohani
- Milango
- Madirisha
- Paa

# HUDUMA ZA NYUMBANI

Kanuni ya Afya inawakataza wamiliki kuzima huduma zinazohitajika za nyumbani, “isipokuwa ni uzimaji wa muda unaoweza kuhitajika wakati matengenezo au mabadiliko halisi yanafanywa au wakati wa dharura za muda.”

Hii inatumika kwa huduma muhimu za nyumbani kama vile gesi, umeme na maji. Haitumiki kwa huduma zisizo muhimu.

## USALAMA WA MOTO

Uwekaji wote wa vigunduzi vya moshi na kaboni monoksidi lazima ufuata Kanuni ya Usalama wa Moto na Majengo, iliyowekwa na Kitengo cha Usalama wa Moto.

### WAJIBU WA MMILIKI

- Vigunduzi vya Moshi na Kaboni Monoksidi.
- Vimeunganishwa kwenye mfumo wa umeme, na vina uwezo wa kutumia betri pia, na vinafanya kazi ipasavyo.
- Angalau kigunduzi kimoja cha moshi na kaboni monoksidi (CO) kwenye ghorofa zote na nje ya maeneo ya kulala.
- Kuanzia tarehe 11/1/2015, vyumba vyote vya kulala lazima viwekwe vigunduzi moshi ambavyo vinaendeshwa kwa umeme na betri pia.
- Ikiwa kitengo cha mfumo wa kuongeza joto kiko kwenye sehemu ya chini ya nyumba, basi vigunduzi vya moshi na CO lazima viweke karibu na chini ya ngazi ya sehemu ya chini ya nyumba.
- Vigunduzi vyote vipya vilivyowekwa vya moshi lazima viwe vya aina inayogundua moshi kwa kutumia mwanga.
- Wapangaji wala sio wamiliki wanahitajika kutoa betri za vigunduzi, lakini ni kwa manufaa ya mmiliki wa mali kuhakikisha kuwa vigunduzi vinafanya kazi ipasavyo.

### KWA KUONGEZEA:

- Kizima moto cha sasa kinachotolewa na mmiliki.
- Njia za kutoka, ikiwa ni pamoja na milango na madirisha ya maeneo ya kulala, zinapaswa kuwa za muundo bora na zisizo na kizuizi.
- Angalau dirisha moja katika vyumba vyote vya kulala na vyumba vinavyotumiwa kama maeneo ya kulala lazima iwe na ukubwa wa kutosha kwa ajili ya kutoka.
- Hakuna vifungo vya ndani vinavyotumia ufunguo wa upande wa ndani kwenye milango ya nje.
- Mifumo ya umeme inatii kanuni.
- Matengenezo ya mifumo ya umeme na kuongeza joto inafanywa tu na fundi aliyeidhinishwa.
- Hakuna nyenzo zinazoweza kuwaka au hatari zilizohifadhiwa kwenye kitengo au karibu na vyanzo vya joto.
- Ngazi za jumla lazima ziwe zimekadiriwa uwezo wake wa kuwaka moto na zisitumike kuhifadhi nyenzo zinazoweza kuwaka.



### WAJIBU WA MPANGAJI

- Usiweke samani za nguo kwenye vibaraza.
- Weka chanja ya nyama choma kwa umbali salama kutoka kwa majengo.
- Jaribu na ubadilisha betri katika vigunduzi vya Moshi na CO mara kwa mara.  
Betri zinapaswa kubadilishwa mara mbili kwa mwaka. Kuzibadilisha unaporekebisha saa zako wakati majira yanapobadilika ni njia nzuri ya kukumbuka.
- Kamwe usiwahi kutenganisha kigunduzi cha moshi au CO.
- Usihifadhi nyenzo zinazoweza kuwaka au hatari kwenye nyumba yako.
- Ripoti matatizo yoyote ya umeme yanayoshukiwa mara moja.

# RANGI ZENYE SUMU YA RISASI

## SUMU YA RISASI

Sumu ya risasi ni tatizo kubwa la kiafya lakini linaloweza kuzuilika. Hakuna kiwango salama cha sumu ya risasi mwilini. Simu ya risasi inaweza kumdhuru mtu yeyote, lakini watoto wachanga, watoto wadogo na wanawake wajawazito wako katika hatari kubwa zaidi. Mtoto anayepata sumu ya risasi huwa haonekani au kutenda kama mgonjwa kila wakati, lakini sumu hiyo ya risasi inaweza kusababisha matatizo makubwa ya kiafya. Madhara yanayotokana na sumu risasi huenda yakadumu maisha yote. Kiwango cha juu cha risasi mwilini, au sumu ya risasi, kwa watoto inaweza kuathiri ubongo, figo na mfumo wa neva, kupunguza kasi ya ukuaji na maendeleo, kufanya iwe vigumu kujifunza, kuharibu uwezo wa kusikia na kuzungumza, na kusababisha matatizo ya kitabia. Watu wazima pia wanakabiliwa na athari mbaya za kiafya kutokana na sumu ya risasi. Kwa wanawake wajawazito, risasi inaweza kuongeza hatari ya kuharibika kwa mimba na kusababisha watoto kuzaliwa mapema sana, wakiwa wadogo sana, au wakiwa na matatizo ya kujifunza au kitabia. Kwa watu wazima, sumu ya risasi inaweza kusababisha shinikizo la juu la damu na kusababisha kupungua kwa uwezo wa kuzaa kwa wanaume.

## SUMU YA RISASI KATIKA MAKAZI

Rangi na vumbi lenye sumu ya risasi kutoka kwa rangi ya risasi ni vyanzo vikuu vya sumu ya risasi kwa watoto. Watoto na watu wazima wanaweza kupata sumu ya risasi wakati wa miradi ya ukarabati au wakati wowote rangi yenye risasi inapong'arishwa, kuondolewa au kuchomwa isivyofaa.

Watoto pia wanaweza kupata sumu ikiwa nyuso zilizopakwa rangi hazitunzwi kwa muda mrefu. Rangi hubambuka na kuwa vumbi linalochafua nyumba na udongo. Vumbi au udongo huu hushikamana na vifaa vya kuchezea, mikono na vitu ambavyo watoto kwa kawaida huweka kwenye midomo yao, na kuwafanya wapate sumu ya risasi. Watoto pia wanaweza kupata sumu ya risasi kwa kula, kutafuna au kunyonya vitu vilivyopakwa rangi ya risasi kama vile sehemu za madirisha au fanicha.

# SHERIA YA SUMU YA RISASI YA VERMONT MBINU ZA UKAGUZI, MATENGENEZO NA USAFISHAJI

Sheria ya Sumu ya Risasi ya Vermont ilipitishwa mnamo 1996 na kurekebishwa mara ya mwisho mnamo 2017 (18 VSA Sura 38). Sheria inawahitaji wapangishaji wa majengo na vituo vya zamani vya matunzo ya watoto kuchukua hatua ili kusaidia kuzuia watoto dhidi ya kupata sumu ya risasi - hatu hizi zinaitwa Mbinu za Ukaguzi, Matengenezo na Usafishaji (IRC) (zilizobadilishwa kutoka “Mbinu Muhimu za Matengenezo (EMP)”) kufikia tarehe 1 Oktoba 2022). Ikiwa mali ya makazi ya kukodisha au kituo cha matunzo ya watoto kilijengwa kabla ya mwaka wa 1978, mmiliki wa mali hiyo au kampuni ya usimamizi wa mali hiyo inahitajika kutii Sheria ya Sumu ya Risasi ya Vermont. Ni lazima:

- Wape wapangaji kijitabu kilichoidhinishwa kuhusu uzuiaji wa sumu ya risasi.
- Wachapishe notisi iliyoidhinishwa inayowaomba watu kuripoti rangi iliyobambuka au iliyoharibika. Angalia [sampuli ya notisi](#) kwenye sehemu ya Zana.
- Wakamilishe mbinu za Ukaguzi, Matengenezo na Usafishaji (IRC) kila mwaka, ikiwa ni pamoja na:
  - Kukagua mali sehemu za ndani na nje.
  - Kutambua maeneo ambayo rangi au mipako iko katika hali mbaya (kubambuka au kumenya) na kuhakikisha imerekebishwa mara moja kwa njia salama inayozingatia sumu ya risasi.
  - Kuthibitisha kuwa madirisha yote ya mbao yaliyowekwa kabla ya mwaka wa 1978 yana vifuniko vya sehemu za chini za madirisha.
  - Kuondoa vipande vyovyote vinavyoonekana vya rangi kwenye ardhi nje ya jengo.
  - Kufanya usafishaji maalum katika maeneo ya jumla.
- Wamesaini taarifa ya utiifu inayothibitisha kuwa Mbinu za IRC zimetetelezwa na utoe nakala kwa wapangaji, mtoa huduma ya bima na Idara ya Afya angalau kila baada ya siku 365.

## UTHIBITISHAJI WA IRC

Mbinu za IRC lazima zitekelezwe na mtu ambaye ameidhinishwa na IRC - huyu anaweza kuwa mpangishaji au msimamizi wa mali. Ili kuthibitishwa na IRC, ni lazima mtu huyo ahudhurie mafunzo ya Mbinu za IRC yaliyoidhinishwa na Idara ya Afya na afanye mtihani. Mafunzo ya Mbinu za IRC hufundishwa ana kwa ana na mtandaoni. Mafunzo pamoja na mtihani huchukua muda wa takriban saa tatu. Pata mafunzo na maelezo zaidi kuhusu masharti ya Mbinu za IRC katika <https://healthvermont.gov/IRC>. Unaweza pia kuwasilisha malalamiko kuhusu ukosefu wa utiifu wa sheria ya sumu ya risasi ya Vermont kwenye sehemu ya chini ya ukurasa wa wavuti.

### MASHARTI YA RANGI ZENYE RISASI KWA MAJUMBA YALIYOJENGWA KABLA YA MWAKA WA 1978

Nyumba zote zilizojengwa kabla ya mwaka wa 1978 zinadhaniwa kuwa na rangi ya risasi ndani au juu yake. Uondoaji wa rangi ya risasi, wakati mwingine huitwa “marekebisho” au “upunguzaji,” hauhitajiki kisheria. Badala yake, ni wajibu wa mpangishaji kudhibiti rangi ya risasi na kufanya urekebishaji au ukarabati wowote kwa njia salama.

## SHERIA YA SUMU YA RISASI YA VERMONT UREKEBISHAJI, UKARABATI, KUPAKA RANGI NA MATENGENEZO

Sheria ya Vermont ilisasishwa hivi majuzi ili kujumuisha masharti ya Ukarabati, Urekebishaji na Upakaji Rangi ya EPA. Hiyo inamaanisha ikiwa mpangishaji anafanya kazi ya ukarabati, urekebishaji, kupaka rangi au matengenezo (RRPM) ambayo inaathiri zaidi ya futi moja mraba ya nyuso zilizopakwa rangi kwa kila chumba cha ndani au sehemu ya nje, kazi hiyo inahitaji kufanywa na mtu binafsi na kampuni yenye leseni zinazofaa za RRPM katika Vermont, na lazima wawape wapangaji taarifa kuhusu kazi wanayofanya na hatari za rangi ya risasi.

Iwe ni mpangishaji, msimamizi wa mali, au mwanakandarasi aliyejiririwa na mpangishaji, ni lazima watumie mbinu za kazi zisizosababisha hatari ya sumu ya risasi kwa kuhakikisha vumbi na uchafu wa risasi unashughulikiwa ipasavyo. Hii ni pamoja na kutumia karatasi za plastiki ili kudhibiti maeneo ya kazi, kuweka ishara za onyo zinazowatahadharisha wengine kuhusu hatari zinazoweza kutokea za sumu ya risasi, kusafisha na kulinda eneo la kazi kila siku, kusafisha maeneo yote ya kazi wakati kazi imekamilika ili kusiwe na vumbi, vipande vya rangi au uchafu katika eneo la kazi.

Zaidi ya hayo, sheria ya sumu ya risasi za Vermont inakataza matumizi ya mbinu zisizo salama za kazi ikiwa ni pamoja na kuondoa rangi yenye risasi kwa kuchoma, kutumia bunduki ya joto, kuosha kwa shinikizo, kukwarua, matumizi ya zana za umeme bila kibali na kutumia kemikali kutenganisha rangi na nyuso. Mbinu hizi zisizo salama za kazi huongeza hatari ya kupata sumu ya risasi.

Pata maelezo zaidi kuhusu masharti RRPM ya Vermont kwenye <https://healthvermont.gov/RRPM>

### MANUFAA YA SHERIA YA RANGI YENYE SUMU YA RISASI

#### HUWALINDA WATOTO

Mbinu rahisi zinazoendelea za matengenezo zitazuia watoto dhidi ya kukabiliwa na sumu ya risasi .

#### HUWALINDA WAMILIKI WA MALI

Wamiliki wa mali wanaotii sheria hupokea ulinzi dhidi ya dhima iliyoongezeka.


#### HUWALINDA WAFANYAKAZI

Sheria ya sumu ya risasi inakataza matumizi ya mbinu zisizo salama za kazi, hatua ambayo hupunguza uwezekano wa wafanyakazi kukabiliwa na sumu ya risasi.

# KUWEKA MALI KATIKA HALI NZURI

## MATATIZO YANAPOTOKEA: MADOKEZO KWA WAMILIKI

- Shughulikia maombi ya matengenezo mara moja.
- Fanya ukaguzi wa mara kwa mara wa nyumba au jengo.
- Tii maombi yote ya ukarabati au amri zinazotolewa na afisa wa jimbo au eneo.
- Uharibifu wa kimakusudi unaweza kuzingatiwa kama uharabu katika hali zingine.
- Wakaguzi wa Afya na Usalama wa Moto wanapatikana kwa wamiliki pia.



## IKIWA MPANGAJI ANAWAJIBIKA KWA KULIPIA HUDUMA MUHIMU ZA NYUMBANI NA HAZITOLEWI.

Iwapo makubaliano ya kukodisha yanamtaka mpangaji kulipia huduma zozote muhimu za nyumbani (JOTO, UMEME, MAJI, UTUPAJI WA MAJI TAKA) na zimezimwa kwa kutolipa, chaguo zako ni pamoja na:

- Wapangaji wamekiuka Kanuni ya Afya na/au Usalama wa Moto. Wakaguzi wa Utekelezaji wa Kanuni, Maofisa wa Afya wa Mji na Wakaguzi wa Usalama wa Afya wanaweza kukusaidia pia!
- Wapangaji wamekiuka makubaliano ya kukodisha. Unaweza kuwapa notisi ya kuondoka kama inavyohitajika na sheria.
- Unaweza kuomba bili itumwe kwa jina lako ili kuepuka ukaribifu (hii ni chaguo, HAIHITAJIKI na sheria).
- Ikiwa wapangaji wamesababisha mfumo wa kuongeza joto kuzimwa katika miezi ya msimu wa baridi na kuna hatari inayowezekana kwa mali yako kutokana na kupasuka kwa mabomba, **UNAWEZA** na sababu ya kisheria ya kuzima mfumo wa maji na kutoa maji kwenye mabomba. **Tafuta ushauri wa kisheria kila mara kabla ya kuchukua hatua hii kwani kuzima huduma muhimu kwa ujumla ni marufuku.**

## MATATIZO YANAPOTOKEA: SULUHU ZA KISHERIA KWA MKODISHAJI

### KUTUMIA SHERIA YA “KUFANYA MATENGENEZO NA KUKATA KUTOKA KWA KODI” KWA MATENGENEZO MADOGO

- Ikiwa matengenezo hayatafanywa baada ya ombi la kwanza, tuma ombi lililoandikwa. **Ni muhimu kuwa na kumbukumbu.**
- Zingatia kutumia sheria ya Vermont ya "Kufanya Matengenezo na Kukata kutoka kwa Kodi"\* kwa matengenezo madogo.
  - Sheria ya kufanya matengenezo na kukata kutoka kwa kodi inahitaji kwamba mpangaji aandike ombi la matengenezo na atoe siku 30 kwa mmiliki ili kufanya matengenezo. Kuna [barua ya kawaida](#) kwa kusudi hili katika sehemu ya “Zana” ya Mwongozo huu.
  - Matengenezo yanayoombwa lazima yawe kitu kinachohitajika ili kutii kanuni za ujenzi, makazi au afya, au “kipengele muhimu cha makubaliano ya kukodisha.”
  - Baada ya siku 30, mpangaji anaweza kuleta fundi afanye matengenezo au afanye mwenyewe na kukata gharama kutoka kwa kodi ya mwezi unaofuata. Wapangaji hawaruhusiwi kukata zaidi ya nusu ya kodi ya mwezi mmoja.
  - Nakala za risiti lazima zitolewe kwa mmiliki.
  - Wapangaji HAWAPASWI wao wenyewe kufanya matengenezo yanayohitaji fundi aliyeidhinishwa, kama vile mifumo ya umeme, kuongeza joto au mabomba.
  - Vibali vinaweza kuhitajika.
- Sheria ya kufanya matengenezo na kukata kutoka kwa kodi pia inaweza kutumika kumfanya mmiliki atii masharti ya mkataba ulioandikwa wa ukodishaji. Kwa mfano, ikiwa mkataba wa ukodishaji unasema kuwa huduma kama vile kuondoa taka, kulima au maegesho zimejumuishwa, lakini hazitolewi, mpangaji anaweza kufanya mipango yake mwenyewe, ikiwa ni pamoja na kulipia maegesho nje ya eneo.

*\*Ikiwa hitaji la matengenezo ni la dharura, kama vile ukosefu wa joto wakati wa msimu wa baridi, au ikiwa matengenezo ni ghali sana, ni bora kutumia chaguo moja au zaidi zilizo rodheshwa hapa chini badala ya kutumia sheria ya kufanya matengenezo na kukata kutoka kwa kodi.*

### MATENGENEZO KWA AJILI YA AFYA NA USALAMA

- Mpigie [Afsa wa Afya wa Mji](#) au Mkaguzi wa Kanuni wa Manispaa ili kuomba ukaguzi wa Kanuni ya Afya ya Makazi ya Ukodishaji. Kaguzi hizi hufanywa bila malipo. Mkaguzi wako ana mamlaka ya kuhitaji Ukiukaji wowote wa Kanuni urekebishwe.
- Nenda kwenye [tovuti ya Kitengo cha Usalama wa Moto cha VT](#) ili kuwasilisha malalamiko ya matatizo ya usalama wa moto, umeme, mabomba.
- Maelezo ya mawasiliano yanapatikana katika sehemu ya nyenzo ya mwongozo huu.

### KUKATAA KULIPA KODI HADI MATENGENEZO YAFANYWE\*

Sheria ya Vermont inaruhuru kukataa kulipa kodi hadi matengenezo yafanywe kwa sababu **moja** pekee— ukiukaji mkali wa kanuni ya afya na usalama wa maisha unaoathiri **afya na usalama muhimu** wa mkodishaji na ikiwa **tu** mkodishaji amechukua hatua zifuatazo:

- Mpangaji lazima ampe mpangishaji noti iliyoandikwa ya tatizo hilo. Inapendekezwa kutuma noti hii kwa barua iliyoidhinishwa.
- Mpangishaji kisha anaruhusiwa muda wa kutosha wa kurekebisha tatizo.
- Muda ambao mpangishaji anapewa ili kufanya marekebisho hutegemea aina ya tatizo. (Sio siku 30 kila wakati.) [9 V.S.A. Sura ya 137, §4458](#)

**\*Kukataa kulipa kodi ni hatua kubwa na haipaswi kuchukuliwa hadi upate ushauri kutoka kwa mwanasheria au wakili mtaalamu wa upangaji mtaalamu. Vermont Tenants huzungumza na watu wengi kila mwaka ambao hawakufuata utaratibu unaofaa na hivyo kufukuzwa kwa sababu hiyo. Ni muhimu kwamba mpangaji awe na pesa za kutosha endapo mpangishaji atianza utaratibu wa kumfukuza. (Angalia [“Kesi za Kulipa Kodi kwa Mahakama Badala ya Mpangishaji”](#))**

#### Mkodishaji anaweza pia:

- Kuvunja mkataba wa ukodishaji kwa kutoa noti inayofaa.
- Kutafuta amri ya kisheria (kupata amri ya mahakama).
- Kufungua mashtaka ya kiraia dhidi ya mpangishaji.

## IWAPO MMILIKI ANAWAJIBIKA KULIPIA MAJI NA BILI HAILIPWI:

- Anza kwa kuwasiliana na [Afisa wa Afya wa Mji](#).
- Ikiwa mmiliki hatafuata maelekezo ya afisa au ikiwa utashindwa kuomba ukaguzi ufanywe, bado una chaguo kadhaa.
- Sheria ilipitishwa mnamo mwaka wa 2015 iliyowapa wapangaji chaguo la kuomba bili ya maji itumwe kwa jina lao ikiwa mmiliki atashindwa kulipa bili na huduma hiyo ikatwe. Inasema hivi:

*Mkodishaji wa makazi ya kukodisha iliyekatiwa huduma kwa sababu ya ukosaji wa mlipa gharama atakuwa na haki ya kuomba na kulipia huduma inayoendelea kutoka kwa huduma au kuunganishwa tena na huduma ya maji na maji taka kwa makazi ya kukodisha, ambayo shirika la huduma litatoa. Iwapo ada au tozo zozote za maji na maji taka zimejumuishwa katika kodi ya mpangaji, mpangaji anaweza kukata gharama ya malipo yoyote ya huduma ya maji na maji taka au ada zinazolipwa kwa manisipaa kutoka kwa kodi yake kwa mujibu wa 9 V.S.A. § 4459. (Kufanya Matengenezo na Kukata Kutoka kwa Kodi) Chini ya hali kama hizi, shirika halitamhitaji mpangaji alipie deni lolote linalozidi mzunguko mmoja wa bili.*

[24 V.S.A. § 5143\(c\)](#)

\*Hii inamaanisha kuwa mpangaji anaweza kuchukua jukumu la kulipia maji, ikiwa malipo ya maji yalijumuishwa kwenye kodi. Kisha anaweza kukata gharama kutoka kwa malipo yake ya kila mwezi ya kodi. Shirika la huduma haliwezi kutoza mpangaji kwa zaidi ya mzunguko mmoja wa bili kwa malipo yaliyochelewa ya bili.

## IKIWA MMILIKI ANAWAJIBIKA KULIPIA HUDUMA MUHIMU (JOTO, UMEME, MAJI, UTUPAJI WA MAJI TAKA) NA HUDUMA HIZI HAZITOLEWI:

- Anza kwa kuwasiliana na Mkaguzi wa Kanuni au Ofisi ya Afya ya Mji wako.
- Ikiwa mmiliki hatafuata maelekezo ya mkaguzi au ikiwa utashindwa kuomba ukaguzi ufanywe, huenda ikawa rahisi kwa wakodishaji kuomba Amri ya Usaidizi wa Dharura mahususi kwa huduma muhimu mahakamani. Wasiliana na [Vermont Tenants](#) au mwanasheria katika hali kama hii.
- Hii ndiyo chaguo bora zaidi katika hali ambapo zaidi ya nyumba moja hutumia huduma na hakuna mita tofauti.

**\* SULUHU ZILIZO HAPO JUU ZA WAPANGAJI HAZIPATIKANI KWA WAPANGAJI IKIWA TATIZO LILISABABISHWA KWA MAKUSUDI AU KWA UTELEKEZAJI WA WAKAAJI AU WAGENI WAO.**



# SEHEMU YA 5: MATATIZO YA KAWAIDA

## MASUALA KATI YA MAJIRANI



Matatizo kati ya majirani yanaweza kuwa changamoto kwa wahusika wote. Wapangaji mara nyingi wanaweza kuhisi kama mmiliki hafanyi chochote kuhusu tatizo hilo na wamiliki wanaweza kujipata wakipokea simu zisizoisha za malalamiko. Kwa kweli, mmiliki hawajibiki kila wakati majirani wanapozozana na huenda asiwe na uwezo wa kutatua kila tatizo.

Ingawa wapangaji wana haki ya “Kufurahia Nyumba kwa Amani” kuna tofauti kubwa kati ya wapangaji wawili wasioelewana na “unyanyasaji.” Unyanyasaji huelekezwa kwa upande mmoja.

Wakati wa kipindi cha mkataba wa ukodishaji, chaguo pekee ambalo mmiliki anaweza kutumia ni kusimamisha upangaji wa mpangaji mmoja au wote wawili wanaozozana, hatua ambayo inaweza kuchukuliwa tu ikiwa mmiliki atashinda kesi ya kufukuzwa ya “Kwa Sababu”. Hii si rahisi kila wakati na hatimaye hakimu ataamua. Hata hivyo, ikiwa wapangaji hawana mkataba wa ukodishaji uliokwekwa kwa kipindi fulani (kwa mfano, kuna mkataba wa kila mwezi au kulikuwa na mkataba wa awali wa ukodishaji wa mwaka ambao uliisha muda wake na haukusasishwa), wapangishaji wengi wanaweza kufanya tu ufukuzaji bila sababu au kwa kutosasishwa ([angalia ukurasa wa 39](#) kwa maelezo).

### MIFANO YA UKIUKAJI WA HAKI YA MPANGAJI YA KUFURAHIA KWA AMANI:

- Kelele nyingi kupita kiasi nyakati fulani zinazotajwa na mji wako kama “saa za kutofanya kelele.”
- Unyanyasaji akiwa katika maeneo ya jumla.
- Vurugu au vitisho kwako au wageni wako.
- Uharibifu wa vitu vyako.

### MADOKAZO KWA WAMILIKI:

- Uliza watu wanaomfahamu!
- Kupata wapangaji ambao wanaweza kuelewana kunaweza kusaidia kuzuia tatizo hili.
- Washirikishe wapangaji wa sasa katika kutafuta wapya. Wape fursa ya kukutana na watu wanaotarajiwa kukaa nao.

### MADOKAZO KWA WAPANGAJI

- Kelele za kawaida na za kila siku sio ukiukaji wa haki zako.
- Jaribu kutatua matatizo kabla ya kumhusisha mmiliki. Sio lazima umhusishe mpangishaji kwenye tatizo la “kutoelewana na” jirani yako.
- Usivutane na majirani wanaokunyanyasa.
- Ikiwa “unawanyanyasa pia” au unapigana nao, unaweza pia kuwa unakiuka makubaliano yako ya kukodisha.
- Ripoti ukiukaji ulioorodheshwa hapa chini kwa mmiliki kwa maandishi.
- Wakati inapofaa, ripoti ukiukaji *mkali* kwa Polisi. Mtumie mmiliki nakala ya ripoti ya Polisi.
- Kuwa na subra. Mmiliki hawezi tu kumfukuza jirani aliyekosea. Hatua ya kufukuza huchukua muda.
- Wasiliana na [Vermont Tenants](#) kwa usaidizi.

## UTUNZAJI WA NYASI NA UONDOAJI WA THELUJI



- Wamiliki hawatakiwi kufanya kazi ya utunzaji wa nyasi au kuondoa theluji isipokuwa iwe imejumuishwa katika masharti ya makubaliano ya kukodisha.
- Wakati kazi ya kuondoa theluji imejumuishwa, kwa ujumla inamaanisha kuondoa theluji kwenye maeneo ya maegesho na njia za kuendesha gari, sio kuiondoa katika kila mlango. Zungumza na mmiliki ili akufafanulie kile atakachofanya na hatafanya.
- Ikiwa kazi ya utunzaji wa nyasi haijajumuishwa katika makubaliano ya kukodisha kwa ujumla ni jukumu la mpangaji.
- Iwapo mali itaachwa ovyo kiasi kwamba inakuwa hatari kwa afya ya umma, Mkaguzi wa Kanuni au Afisa wa Afya wa Mji anaweza kumtaka mmiliki aisafishe. Katika tukio hili, ikiwa kazi ya utunzaji wa nyasi ilikuwa jukumu la mpangaji, mmiliki anaweza kumtoa mpangaji kwa gharama zilizotumika.

## MAEGESHO

- Wamiliki hawatakiwi kutoa maegesho isipokuwa ikiwa imejumuishwa katika masharti ya makubaliano ya kukodisha.
- Ni halali kwa wamiliki kuwatoza wapangaji kwa nafasi ya kuegesha, isipokuwa kama imeainishwa kama “Maegesho ya Walemavu.”
- Ikiwa maegesho yamejumuishwa katika mkataba ulioandikwa wa ukodishaji na hayatolewi, wapangaji wanaweza kutumia sheria ya “[Kufanya Matengenezo na Kukata Kutoka kwa Kodi](#)” ili kumfanya mpangishaji atii mkataba wa ukodishaji.



## DISHI ZA SETILAITI NA ANTENA ZA RUNINGA

Ingawa huduma hizi hazishughulikiwi katika sheria za mpangaji na mpangishaji ya Vermont, zinashughulikiwa na kanuni za FCC.

[Hati ya ukweli inayotolewa na FCC](#) kuhusu uwekaji wa antena na dishi za setilaiti inaweza kupatikana kwenye sehemu ya “Zana” ya Mwongozo huu.



# KULIPISHWA BILI YA HUDUMA ZINAZOTUMIWA

Kulipia Huduma ya Nyumbani Inayotumiwa na Watu Wengine Pia ni maneno yanayotumiwa kuelezea hali ambapo mpangaji analipia huduma ya nyumbani nje ya nyumba yake. Hii inajumuisha maeneo ya jumla, nyumba zingine, au maeneo yanayotumiwa na mmiliki pekee kama vile majengo ya nje au makazi au biashara yake mwenyewe. Ikiwa mpangaji anafikiri kuwa huenda analipia huduma za nyumbani ambazo hatumii, anapaswa kuanza kwa kuzungumza na mmiliki. Ikiwa tatizo halitaweza kutatuliwa, anaweza kutumia chaguo hizi:

## CHAGUO ZINAZOPATIKANA KWA WAPANGAJI

- Mafundi wengi walioidhinishwa wa Umeme hawataweka mfumo kama huo wa kuunganisha waya. Iwapo unafikiri kazi ya umeme imefanywa na mtu asiyeidhinishwa, wasiliana na Idara ya Usalama wa Umma ya Vermont, [Kitengo cha Usalama wa Moto](#) ili kazi hiyo ikaguliwe kwa usalama na utiifu wa kanuni za umeme. Pata nakala ya ripoti ya ukaguzi huo.
- Manispaa zilizo na Ofisi zao za Utekelezaji wa Kanuni pia zinaweza kutekeleza baadhi ya kanuni za usalama wa moto.
- Iwapo ukaguzi utaonyesha kuwa unalipia huduma zilizo katika maeneo nje ya nyumba yako, unapaswa kukadiria malipo yako na utume bili kwa mmiliki.
- Ikiwa hali hii haiwezi kutatuliwa, unaweza kufungua mashtaka katika mahakama ya madai madogo.
- Ikiwa unashuku unalipia huduma katika maeneo ambayo hayapo katika nyumba yako, lakini hakuna ukiukaji wa kanuni ya umeme au usalama wa moto, ambao unahitaji ukaguzi rasmi, unaweza kuajiri fundi umeme wako mwenyewe na uweke kumbukumbu ya kazi unayolipia na utumie kumbukumbu hizi katika mahakama ya madai madogo.

## MADOKAZO KWA WAMILIKI

- Huduma za nyumbani katika kila nyumba zinapaswa kuwekewa mita tofauti. Maeneo ya jumla yanapaswa kuwa na mita zake na ulipishwe bili zake.
- Ikiwa haiwezekani kuweka mita binafsi, huduma hiyo inapaswa kujumuishwa kwenye kodi.
- Ni kinyume na sheria kwa mmiliki “kuuza tena” huduma inayodhibitiwa ya umma kwa wapangaji wake. Huduma zinazodhibitiwa ni pamoja na maji, umeme, na gesi asilia ya bomba.

## VIFAA VYA NYUMBANI

- Wamiliki hawatakiwi kutoa vifaa kama vile jiko na jokofu.
- Ikiwa vifaa vinatolewa, mmiliki ana wajibu wa kuviweka katika hali nzuri ya kufanya kazi.
- Mmiliki anaweza kuepuka jukumu la kutunza vifaa kwa kuweka kifungu katika mkataba wa ukodishaji kinachosema kwamba hatoi uwakilishi wowote kuhusu hali ya vifaa, na kinachosema wazi kwamba mpangaji anawajibika kwa matengezo yote ya vifaa.
- Ikiwa mmiliki hatarekebisha kifaa kilichoharibika ambacho anawajibika, mpangaji anaweza kukirekebisha na akate gharama kutoka kwa kodi. Angalia “[Kufanya Matengenezo na Kukata Kutoka kwa Kodi](#)”, kwa njia inayofaa ya kufanya hivi.

# SEHEMU YA 6: KUHAMA

## KUVUNJA MKATABA WA UKODISHAJI

Mkataba wa ukodishaji ni mkataba unashurutisha kisheria. Adhabu za kifedha kwa mpangaji kwa kuvunja mkataba wa ukodishaji zinaweza kuwa kubwa.

Sheria ya Vermont inamruhusu mmiliki kumwajibisha mpangaji kulipia gharama za mkataba wa ukodishaji hadi nyumba itakapokodishwa tena. Pia inaruhusu mmiliki kumtoza mpangaji kwa gharama zinazofaa zinazohusika katika kukodisha tena.

### SABABU ZA KISHERIA ZA KUVUNJA MKATABA WA UKODISHAJI

- Ukiukaji Mbaya wa Kanuni ya Afya au Usalama wa Maisha ambao unaweka katika hatari afya au usalama wa wakaaji lakini **LAKINI BAADA TU YA:**
  - Mpangaji ametuma noti iliyoandikwa ya tatizo kwa mmiliki.  
NA
  - Mmiliki ameruhusiwa kipindi “kinachofaa” ili kurekebisha tatizo.
  - Ikiwa tatizo halitatatuliwa, mpangaji bado lazima atoe “notisi inayofaa” ya kuhama.
- Mpangaji akiitwa kwa kazi ya kutumikia Jeshi.
- Kama sehemu ya ombi la Marekebisho Yanayofaa la mpangaji aliye na ulemavu.
- Kama sehemu ya ulinzi unaotolewa kwa waathiriwa wa dhuluma za kinyumbani, unyanyasaji wa kingono na unyatiaji chini ya sheria ya ubaguzi wa makazi ya Vermont.

### WAPANGAJI WANAOFIKIRIA KUVUNJA MKATABA WA UKODISHAJI WANAPASWA KUPATA USHAURI WA KISHERIA KABLA YA KUFANYA HIVYO!

### MADOKAZO KWA WAMILIKI

- Tumia mkataba ulioandikwa kwa ukodishaji.
- Fahamu kwamba mpangaji anaweza kuondoka wakati wowote, lakini ikiwa una mkataba wa ukodishaji wa muda mrefu mpangaji anaweza kuwajibika kifedha kwa muda uliosalia wa mkataba wa ukodishaji.
- Ikiwa mpangaji atahama mapema, mpangishaji ana wajibu wa kisheria wa kujaribu kukodisha tena nyumba.



# MASHARTI YA NOTISI YA WAPANGAJI WANA OHAMA

- **Sheria sio notisi ya siku 30, ni:**
  - Notisi iliyoandikwa isiyopungua Kipindi Kimoja Kamili cha Kukodisha.
  - Iwapo kodi inalipwa tarehe moja, notisi inapaswa kutolewa kufikia siku ya mwisho ya mwezi ili kuhama kufikia siku ya mwisho ya mwezi wa notisi.
  - Mfano: Unatoa notisi mnamo au kabla ya tarehe 30 Juni, muda wa notisi yako ni mwezi wa Julai. Utahama usiku wa manane tarehe 31 Julai.
- Notisi iliyo hapo juu inatumika isipokuwa kama imeandikwa vinginevyo katika mkataba wa ukodishaji. Ikiwa mkataba wa ukodishaji unasema siku 30, unapaswa kutoa notisi kama hiyo, na notisi ya kuhama katikati ya mwezi inaruhusiwa. Ikiwa mkataba wa ukodishaji unahitaji muda mrefu wa notisi, lazima utoe notisi kwa muda uliotajwa ndani yake. Hii hutumika hata kama muda wa mkataba wa ukodishaji umeisha.
- Sheria za Jiji la Burlington zinahitaji mpangaji anayekusudia kuhama kutoa notisi ya Vipindi VIWILI Kamili vya Kukodisha, isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo katika mkataba wa ukodishaji.
- Wamiliki wanaweza kukata kutoka kwa amana ya dhamana kwa notisi isiyotosha ikiwa watapoteza mapato ya kukodisha.

## MADOKEZO KWA WAMILIKI:

- Ikiwa mpangaji atakupa notisi ya mdomo kwamba anahama, omba aiweke katika maandishi.
- Ikiwa mpangaji anahama kabla ya mwisho wa muda wa mkataba wa ukodishaji, hakikisha kuwa umejaribu kukodisha tena nyumba.
- Muda wa kurejesha amana ya dhamana huanza kufanya kazi kuanzia tarehe ambayo mpangaji atahama, na sio mwisho wa mkataba wa ukodishaji au kipindi cha notisi.

## MADOKEZO KWA WAPANGAJI

- Tumia sampuli ya [Notisi ya Kuhama](#) inayotolewa katika sehemu ya “Zana” katika Mwongozo huu.
- Toa notisi yenye muda wa kutosha iwezekanavyo zaidi ya masharti ya kisheria.

# MATARAJIO YA HALI WAKATI WA KUHAMA

Inapendekezwa sana kwa wapangaji kuacha nyumba katika hali waliyoipata. Uchakavu wa kawaida unapaswa kutarajiwa na gharama zake hazipaswi kukatwa kutoka kwa amana ya dhamana. Matengenezo ya kawaida yanayofanywa wakati wa kukodisha tena yanapaswa kuwa jukumu la mmiliki, sio mpangaji.

## MADOKEZO KWA WAMILIKI:

- Piga picha za uharibifu wowote.
- Kagua hali ya nyumba kwa kutumia [orodha hakikishi iliyoandikwa](#) (inapaswa kuwa fomu sawa na iliyotumiwa wakati kwa kuhamia).
- Haihitajiki kwamba mpangaji awepe kwa ukaguzi wa kuhama.

## MADOKEZO KWA WAPANGAJI

- Mwambie mmiliki akague hali ya nyumba pamoja nawe wiki 2 hadi 3 kabla ya kuhama. Mwambie akueleze matengenezo yoyote anayohisi ni jukumu lako.
- Ikiwa huna uhakika kama matengezo ni jukumu lako au la, pigia simu [Vermont Tenants](#) kwa usaidizi.
- Piga picha baada ya kuondoa vitu vyako na kusafisha nyumba.
- Unawajibika kwa uharibifu unaosababishwa na wageni au ajali.

# MAREJESHO YA AMANA YA DHAMANA NA MIGOGORO

Mara nyingi mizozo ya amana husuluhishwa katika Mahakama ya Madai Ndogo.\* Ni vyema kwa wahusika wote kuwa na hati wazi ya hali ya nyumba wakati wa kuhamia ili kuepuka hatua ya mahakama au kama ushahidi ikiwa mashtaka yatahitajika ili kusuluhisha kutokubaliana.

\*Katika Burlington, Bodi ya Ukaguzi wa Makazi inaweza kutumika badala ya Mahakama ya Madai Ndogo.

## MAREJESHO YA AMANA

- Chini ya sheria ya Vermont, ni lazima wamiliki warejeshe amana, ikijumuisha kutoa rekodi ya makato yoyote, ndani ya siku 14 baada ya siku ambayo mpangaji atawajulisha kuwa amehama au inapogundulika kuwa amehama.
- Siku 14 huanza siku moja baada ya mpangaji kuhamia nyumba, bila kujali tarehe iliyowekwa katika notisi.
- Amana lazima ziwekwe alama ya posta ndani ya siku 14, si lazima zimfikie mpangaji kwa wakati huo.
- Ikiwa mmiliki hajui anwani mpya ya mpangaji, amana inapaswa kutumwa kwa anwani ya mwisho inayojulikana (nyumba ambayo ambacho mpangaji amehama hivi majuzi).

## MIGOGORO YA AMANA

- Ikiwa mmiliki atashindwa kurejesha amana kwa mpangaji katika muda unaohitajika, atapoteza haki yake ya kukata gharama kutoka kwa amana hiyo na atapaswa kurejesha amana kamili. Hii haimaanishi kuwa mpangaji bado havezi kuwajibika kwa pesa zozote zinazodaiwa kwa uharibifu, huduma za nyumbani au kodi isiyolipwa. Mmiliki anaweza kufungua kesi katika Mahakama ya Madai Madogo.
- Wamiliki wanaweza kutoza pesa zinazodaiwa na uharibifu zaidi ya kiasi cha amana.
- Ikiwa mmiliki atazuia amana kwa makusudi anaweza kuwajibika kurejesha kiasi cha amana mara mbili kulingana na mahakama ya Madai Madogo au na Bodi ya Ukaguzi ya Makazi. Ni jukumu la mpangaji kuthibitisha umakusudi.

## VITU VILIVYOACHWA NYUMA BAADA YA KUHAMIA

Hii inatumika **tu** kwa vitu vilivyoachwa nyuma katika nyumba ya kukodisha baada ya;

- Mpangaji kutoa notisi kwa mmiliki kwamba wapangaji wamehama, au
- Baada ya mpangaji kuhamia mwishoni mwa muda wa mkataba wa ukodishaji.

[9 V.S.A. §4462\(d\)](#): *Vitu vyovyote vya binafsi vilivyobaki katika nyumba ya makazi au jengo lililokodishwa baada ya mpangaji kuhamia vinaweza kutupwa na mpangishaji bila notisi au dhima kwa mpangaji au mmiliki wa vitu hivyo vya binafsi.*

\*Kwa vitu vilivyoachwa nyuma baada ya kufukuzwa rejelea ukurasa wa [46](#)

\*Kwa vitu vilivyoachwa nyuma wakati nyumba imeachanishwa rejelea ukurasa wa [47](#)



# WATU WANAOMFAHAMU

Hakuna sheria za mpangishaji na mpangaji zinazoshughulikia kile ambacho mpangishaji anaweza au hawezi kusema anapooombwa kutoa marejeleo kuhusu watu wanaomfahamu mpangaji. Watu wanafahamu mtu wanaweza kushughulikiwa na sheria za kashfa (zilizoandikwa) na kashfa (za maneno) ikiwa taarifa iliyotolewa si ya kweli. Sheria hizi mbili pia zinaweza kutumika kwa maoni yanayotolewa na wapangaji kuhusu wamiliki.

## WAKODISHAJI: IKIWA UNADHANI MPANGISHAJI WA AWALI ANAWEZA KUTOA MAONI YASIOFAA KUKUHUSU:

- Huenda ukaamua kumwacha mpangishaji huyo nje ya orodha. Hata hivyo, ukimwacha mpangishaji na kisha wakala wa nyumba au mwenye nyumba yenye ruzuku agundue kuhusu mpangishaji huyo, unaweza kunyimwa nyumba kwa msingi wa ulaghai au kukosa kutoa taarifa kamili kuhusu ombi lako la makazi.
- Jaribu kuzungumza na mpangishaji wako wa awali. Mwombe akupe maoni ya kukufahamu rahisi yanayoangazia ulichofanya vyema, kama vile kulipa kodi kwa wakati.
- Mwonyeshe kuwa hali zimebadilika, kwa mfano:
  - Hukulipa kodi kwa kipindi fulani cha muda kwa sababu ya hali mbaya ya nyumba.
  - Kusanya picha, ripoti za bodi ya afya, au taarifa kutoka kwa watu walioona hali ya nyumba hiyo.
  - Tatizo la kiafya au la kifedha ambalo lilikufanya uchelewe kulipa kodi yako ambalo kwa sasa limetatuliwa.
  - Usumbufu katika nyumba yako ulitokea kwa sababu ya dhuluma iliyofanywa dhidi yako. Kusanya taarifa za washauri waliojua kuhusu hali yako, ripoti za polisi, au amri za kuzuia.
  - Umepata nyumba mpya ambayo inaruhusu mnyama kipenzi ambaye alifanya ukiuke kanuni ya kutoruhusu mnyama kipenzi.
  - Sasa unapokea huduma za kijamii ambazo zitakuwezesha kutii mkataba wako wa ukodishaji.
- Fikia njia nyingi za kufanya hivi: je, nani mwingine anaweza kutoa maoni ya kukufahamu? Zingatia maoni ya watu wa karibu, waajiri, walimu, majirani, wasimamizi wa kesi, na viongozi wa kidini.
- Kuna njia zingine za kuthibitisha uwajibikaji wa kifedha. Kuwa na akaunti ya kuweka na kutoa pesa na ya akiba kunaonyesha kuwa unaweza kudhibiti pesa zako au kuwa na mdhamini kunaweza kusaidia uamuzi wa mpangishaji kuhusu nani wa kukodisha.

## MADOKEZO KWA WAMILIKI:

- Kuwa mkweli.
- Tumia taarifa zinazoweza kuthibitishwa na uepuke maoni ya binafsi.

## MADOKEZO KWA WAPANGAJI

- Maoni mabaya ya kufahamu mtu itafanya iwe vigumu kupata nyumba mpya.
- Kuwa mpangaji anayewajibika – lipa kodi kwa wakati, fuata masharti ya kukodisha, na utunze mali.
- Ikiwa una sababu ya kuamini maoni ya kukufahamu hayatakuwa mazuri, kuwa mkweli kwa mpangishaji unayetaka kukodisha kutoka. Kila wakati ni bora kujieleza mapema kuliko kushangazwa wanapompigia simu mmiliki wa ukodishaji wako wa sasa.



# SEHEMU YA 7: USIMAMISHAJI WA UPANGAJI NA MMILIKI

## USIMAMISHAJI WA UKODISHAJI KWA KUTOLIPA KODI

Notisi ambayo mmiliki anatoa kwa mpangaji ili kusimamisha upangaji wa mpangaji kwa kutolipa kodi lazima itimize masharti fulani chini ya sheria ya Vermont. Notisi hiyo lazima:

- Iwe imeandikwa na iwasilishwe kwa mkono au kwa barua kwa mpangaji (barua pepe, SMS, na jumbe za Facebook hazizingatii sheria).
- Ipokelewe na mkodishaji.
- Impe mpangaji angalau siku 14 za kulipa kodi (bila kujumuisha siku ambayo notisi ilitolewa).
- Ijumuishe kiasi mahususi cha deni inayodaiwa ya kodi (usijumuishe ada za kuchelewa, huduma za nyumbani ambazo hazijalipwa wala amana ya dhamana ambayo haijalipwa).
- Itoe tarehe ya mwisho ya kuhama.
- Imwambie mpangaji ikiwa atalipa kodi ndani ya siku 14, notisi hiyo itaondolewa.

*Ikiwa notisi ya kusimamisha upangaji haizingatii masharti haya, kesi ya mahakama inaweza kutupiliwa mbali.*

### MADOKEZO KWA WAPANGAJI

- Iwapo unajua huenda usiweze kulipa kodi, zungumza na mpangishaji kabla ya muda wa kulipa kufika.
- Jitahidi kulipa kiasi kingi zaidi uwezavyo siku ya kwanza na umpe mmiliki tarehe madhubuti katika mwezi utakapolipa salio.
- **Usimtoroke mmiliki!** Utafanya tu hali hiyo kuwa mbaya zaidi.
- Ukipokea notisi, wasiliana na ofisi ya Shirika la Usaidizi wa Jamii iliyo karibu nawe na uulize kama kuna mipango katika eneo lako inayosaidia kwa madeni ya kodi.
- Ikiwa ulikuwa umeacha kulipa kodi kwa sababu ya matatizo ya nyumba, lazima uwe umechukua hatua sahihi (angalia [Kukataa Kulipa Kodi](#) kwenye ukurasa wa 28). **Lazima bado ulipe deni hilo!** Kuna uwezekano utaamrisha kulipa katika akaunti ya mahakama wakati wa utaratibu wa kufukuzwa. Ikiwa huna, mmiliki anaweza kupata hati muhimu ili kukufukuza haraka zaidi. (Angalia [Kesi za Kulipa Kodi kwa Mahakama Badala ya Mpangishaji](#) kwenye ukurasa wa 44)
- Ikiwa unahitaji usaidizi kuunda bajeti, [Mipango ya Mashirika ya Usaidizi wa Jamii](#) hutoa huduma za ushauri wa kifedha.

### MADOKEZO KWA WAMILIKI

- Kuna [sampuli ya notisi](#) kwenye sehemu ya “Zana” katika Mwongozo huu. **Usiibadilishe, unaweza kusababisha kesi hiyo itupiliwe mbali!**
- Kusubiri hadi mpangaji awe na madeni ya miezi mingi ya ukodishaji sio hatua nzuri. Kunaweza kuwa na huduma za msaada zinazopatikana kwa mpangaji, lakini si kama kiasi kinachodaiwa ni zaidi ya miezi miwili ya deni ya kodi.
- Msaada wa deni la kodi unahitaji kwamba mpangaji awe na notisi iliyoandikwa ya kusimamishwa kwa upangaji.
- Dhana kwamba inachukua miezi mingi kumfukuza mpangaji kwa ujumla husababishwa na mmiliki kusubiri kwa muda mrefu kabla ya kutuma notisi. Ukifuata utaratibu ufao suluhu litapatikana haraka.



# NOTISI YA USIMAMISHAJI “KWA SABABU FULANI”

Kusimamishwa kwa upangaji “kwa sababu fulani” kunamaanisha kuwa mmiliki anataka wakaaji wahame kwa sababu wamekiuka masharti ya makubaliano ya kukodisha au wamekiuka sheria ya mpangaji na mpangishaji au kanuni za eneo.

Mifano ni pamoja na:

- Wapangaji wanaowaruhusu wengine kuishi nao bila idhini ya mmiliki.
- Kuwasumbua majirani.
- Kuharibu mali kimakusudi. (Hii pia inaweza kuchukuliwa kuwa uharabu chini ya sheria za uhalifu.)
- Kukiuka kanuni za Afya au Moto.
- Kukosa kufuata masharti yaliyowekwa kwenye mkataba wa ukodishaji.

Notisi ambayo mmiliki anatoa kwa mpangaji ili kusimamisha upangaji wa mpangaji kwa sababu fulani lazima itimize masharti fulani chini ya sheria ya Vermont.

Notisi hiyo lazima:

- Iwe imeandikwa na iwasilishwe kwa mkono au kwa barua kwa wapangaji (barua pepe, SMS, na jumbe za Facebook hazizingatii sheria).
- Ipokelewe na mkodishaji.
- Itaje sababu ya kusimamishwa kwa mkataba.
